Nipashe
Jumatatu Agosti 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579994
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



# Aliyefungwa miaka 30 kwa madai ubakaji aachiwa huru

UKURASA 4


Nipashe Spotika
KLABU EPL ZILIVYOTUMIA FEDHA KWENYE USAJILI UK.20
ISIKUPITE
HAT-TRICK...

UKURASA 13

# JPM: Tusihukumu

## MAJALIWA kuunda tume, vifo vyafikia 71, vilio vyatawala kuzika miili...

*Endelea ukurasa wa 2 & 3*



Rais John Magufuli akiwajulia hali majeruhi wa ajali ya moto ambao wamelazwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili baada ya kusafirishwa kutokea mkoani Morogoro. **PICHA: IKULU**



Askari Magereza wakiendelea na shughuli ya kuchimba makaburi katika eneo la Kola Manispaa ya Morogoro ili kuzika miili 65 ya waliofariki baada ya kuungua kutokana na mlipuko wa moto baada ya gari la mafuta kuanguka. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# ...Amlipia bili ya hospitali mil. 5/- aliyefiwa na mama mzazi

UKURASA 2

## Ni wiki ya pilikapilika mkutano SADC Dar

UKURASA 4

MICHEZO **TANZANITE MABINGWA WAPYA COSAFA U-20** UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# ... Amfuta machozi kwa mil. 5/-aliyefiwa na mama mzazi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, jana alimfuta machozi mama aliyefiwa na mama yake mzazi na kushindwa kumudu gharama za matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Ikiwa kama ni muujiza, mama huyo aliyekuwa kwenye korido za kutokea Wodi ya Mwaisela alikuwa amekaa chini na alipomwona Rais anapita alinyoosha mkono akilia kuomba msaada.

Rais Magufuli alisimama kumsikiliza mama huyo ambaye alipaza sauti kueleza msaada anaohitaji na ndipo Rais alimfuta machozi mama huyo.

"Baba nimefiwa na mama yangu, hapa nilipo sina baba sina mama, alisema na Rais Magufuli alimuuliza mama amefariki lini?

"Mama amefariki saa sita usiku wa leo sina hela za kuchukua mwili," alisema huku Rais akimuuliza unadaiwa shilingi ngapi? Na kabla hajajibu karatasi ya bili aliyokuwa nayo ilichukuliwa na Meneja Mawasiliano wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Aminiel Eligeisha, ambaye alitaja kiwango cha fedha.

Baada ya kutajwa kiwango hicho mama huyo alisikika akisema: "Ninadaiwa shilingi milioni tano ambazo sijawahi kuzishika toka nizaliwe, nisaidie baba."

Aidha, Rais alimgeukia Mkurugenzi Mtendaji wa (MNH), Prof. Lawrence Museru, na kumwambia: "Profesa mshughulikie hii halafu mtanidai mimi."

Baada ya maelekezo hayo Rais alimgeukia aliyefiwa na kusema: "Mama hii hapa Sh. 500,000 ikusaidie mama."

# Majeruhi amwomba kitambulisho JPM

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kile kinachoonekana kuwa kuna tatizo la upatikanaji wa vitambulisho vya uraia, jana mmoja wa majeruhi wa ajali ya moto mkoani Morogoro aliyelazwa Muhimbili alisahau maumivu na kukumbuka kitambulisho cha Taifa kwa Rais John Magufuli.

Alivyosikia sauti ya Rais Magufuli akisalimiana na mgonjwa mwingine, aliita 'Magufuli Baba', Rais akaitika; "Ndiyo nakuja baba" na alivyofika alimuuliza jina lake.

Alisema anaitwa Ally Mtita na alikutwa na dhahama hiyo akiwa anapita njia kwenda kwenye shughuli zake, na ndipo Rais alimpa pole.

"Kwanza nakukubali sana kiongozi wangu," Rais akamuuliza na wewe ulikuwa kwenye moto, akajibu: "Nilikuwa kwenye moto bahati au nzuri nilikuwa napita tu moto ukanifuata.

"Ila mimi nina kitu kimoja nataka utusaidie, vile vitambulisho vya Nida."

Rais alimwambia apone kwanza halafu atashughulikiwa, lakini mgonjwa aliendelea kusisitiza kuwa upatikanaji wake umekuwa wa shida sana.

Alimpa fedha, huku Mtita akisisitiza sana kumuelewa na kumkubali Rais Magufuli.

Hivi karibuni, Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema serikali inaboresha mifumo ili kuharakisha utoaji wa vitambulisho vya taifa.

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na misururu mirefu ya wananchi wanaotafuta vitambulisho vya Taifa kutokana na mabadiliko ya kuvitambua kama vitambulisho rasmi kwenye usajili wa laini za simu, kuomba uwakala na huduma nyinginezo muhimu.

Kwenye ofisi mbalimbali za Nida kuna foleni ndefu za wananchi wanaofuta huduma hiyo, huku wengine wakichukua zaidi ya miezi minne kupata vitambulisho hivyo.



Baadhi ya waombolezaji wakimsikiliza Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati alipozungumza baada ya kushiriki k
ilopinduka na kushika moto kwenye eneo la Msamvu mjini Morogoro. Alizungumza na waombolezaji hao, kwenye

# JPM: TUSI

**Na Salome Kitomari**

RAIS John Magufuli amewaasa Watanzania kuacha kutoa hukumu kwa tukio la ajali ya gari la tangi la mafuta iliyotokea juzi eneo la Msamvu, mkoani Morogoro na kuteketeza maisha ya watu kwa moto na wengine kujeruhiwa.

Amesema sio kila aliyekutwa na ajali hiyo alikwenda kuiba mafuta.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo jana alipotembelea majeruhi wa ajali hiyo waliohamimishiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kuwajulia hali na kuwapa pole.

"Tusiwe wepesi wa kuhukumu, kutoa hukumu ni kitu kibaya! Tuvumilie! Hili lingeweza kumpata mtu yeyote, tushikamane katika hili, tumtangulize mbele Mungu, ni majaribu ya shetani na siku zote shetani atashindwa nasi tuendelee kuwa taifa moja," alisema huku wananchi wakiitikia, amina.

"Niwaombe Watanzania tuendelee kuwaombea huu si wakati wa kuwalaumu, kwasababu nimekuwa nikisia baadhi ya watu wakisema kuwa walikwenda kuiba mafuta. Nimemuona dereva alisimamisha gari kwenda kumsaidia mwenzake, amefika moto ukalipuka, mwingine alikuwa anasafiri kwenda Mtwara amezuiwa moto ukalipuka akaungua," alibainisha.

"Niwaombe sana sana Watanzania wenzangu tusiwe na majibu ya haraka, hii ni kazi ya Mungu tujitahidi kuwaombea wagonjwa na marehemu wapumzike kwa amani," alisema na kuongeza:

"Sisi tusiwe majaji kwasababu si kila aliyekuwapo pale aliwenda kuchukua mafuta, wapo waliokwenda kuokoa, wapita njia na safari zao wakapatwa na dhahama hizo," alisema.

Kufuatia ajali hiyo, Rais Magufuli amesema serikali itagharamia matibabu ya majeruhi wote huku akitoa Sh. 500,000 kwa kila mgonjwa aliyekuwa anajitambua na Sh. milioni moja kwa wagonjwa wengine huku Sh. milioni mbili akitoa kwa kwa wauguzi, manesi na madaktari.

Katika kila wodi aliyoitembelea Rais Magufuli alikwenda katika kila kitanda na kutoa pole ya maneno ya faraja pamoja na fedha, huku akiongea na wagonjwa, kuuliza majina yao na kwa wale wasiojiweza alitaka kutajiwa majina yao.

Aliwatembelea majeruhi katika wodi za Mwaisela, Sewahaji, Chumba cha Wagonjwa Mahututi na chumba cha dharura, na baadaye alizungumza na wananchi waliokusanyika nje ya hospitali hiyo.

Rais aliwapongeza wauguzi na madaktari kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuokoa maisha ya watu na kuwaomba Watanzania kuendelea kuwaombea kwasababu wengi wamepata majeraha makubwa ya kuungua.

**SERIKALI KUGHARAMIA MATIBABU**

Rais Magufuli aliagiza majeruhi wote wahudumiwe kwa gharama yoyote na serikali itagharamia matibabu yote kwa sababu ni Watanzania maskini ambao hawakuitaka ajali na kwamba imetokea kwa bahati mbaya.

Baadaye Rais Magufuli aliongea na ndugu wa majeruhi hao na kuwasihi wamtangulize Mungu na kuwaombea na kurudia kusisitiza watu kuacha kuhukumu.

"Niwaombe Watanzania kazi ya

## HABARI KITAIFA



atika maandalizi ya kutambua miili na mazishi ya watu 69 waliofariki dunia katika ajali ya lori la mafuta lil- viwanja vya Hospitali ya Mkoa wa Morogoro, jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# HUKUMU

ajali tusiwe wepesi wa kuhumu, nimeona watu ambao hata si wa Morogoro akiwamo dereva wa gari jingine aliyekwenda kutoa msaada na aliyekuwa anasafiri kwenda Mtwara," alisema.

Awali, Daktari bingwa wa magonjwa ya dharura, Juma Mfinanga, alisema walipokea majeruhi 46, kati yao watatu walifariki, wanane wamelazwa Chumba cha uangalizi maalumu (ICU) wakisaidiwa kupumua kwa mashine baada ya kupata madhara kwenye mapafu, na wengine wameungua zaidi ya asilimia 70 hadi 100.

Alisema majeruhi wengine wamelazwa chumba cha dharura na wengi wameungua kwa zaidi ya asilimi 80.

"Sisi kama wauguzi tunafanyakazi kwa kila hali kuwahudumia kuhakikisha wanarejea kwenye hali zao. Majeruhi 15 ambao wameungua chini ya asilimia 10 wamebaki Morogoro kwa kuwa baada ya tathimini yetu tumeona

INAENDELEA UK.26

# Serikali yaunda tume, majeruhi wafikia 71

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeunda tume ya wataalamu kuchunguza ili kujiridhisha na masuala yanayoacha maswali mengi kwa mamlaka mbalimbali kama ziliwajibika ipasavyo.

Aidha, tume hiyo ilianza kazi jana na itapaswa kutoa taarifa Agosti 16, mwaka huu, ambayo itawekwa wazi kwa wananchi wote.

Alisema hayo jana alipozungumza na maelfu ya wananchi waliojitokeza kuaga miili ya watu 69 waliopoteza maisha kutokana na kulipuka kwa lori la mafuta kwenye eneo la Itigi Msamvu mkoani Morogoro, baada ya gari la mafuta la kampuni ya Chesco ya wilayani Mafinga kuanguka, huku watu wakichota mafuta na baadaye lilipuka.

**WALIOKUFA WAFIKIA 71**

Aidha, waliofariki wamefikia 71 baada ya majeruhi watatu kati ya 59 waliosafirishwa kupelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kufariki kabla ya kupatiwa matibabu.

Alisema kuna maswali mengi ambayo yanapaswa kujibiwa kwenye uchunguzi huyo.

Alisema ajali hiyo imetokea katikati ya manispaa majira ya saa mbili asubuhi ambayo watu walikuwa kwenye majukumu.

"Tunataka tujiridhishe ajali ilipotokea kila mmoja na majukumu yake aliwajibika? Ni mahali palipo na shughuli nyingi za kijamii ikiwamo kituo cha mabasi kuna trafiki, kuna polisi wa ulinzi. Ilipoanguka tu nani alijitokeza kwanza?" Alihoji huku akishangiliwa.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, maswali ni kama waliotangulia mbele ya haki walikuja na magaloni kwenda kuchota mafuta, na je, kwamba walijua lori litaanguka wasubiri au walikuwa na taarifa walipoona limeanguka walikimbilia nyumbani?

"Au wengine walipoona wakakimbia nyumbani kuchukua dishi, kuchukua dumu na kuanza kurudi kwenye gari, huu muda uliopotea na kuwapoteza watu wote waliopotea mbele ya haki ni nani aliwajibika kuwazuia.

Alisema katika eneo ambalo trafiki wanakuwapo kwa wingi na haraka ni ajali inapotokea wanawahi hata kwa gari ya kukodi, hivyo tume itajiridhisha kama walikwenda kwa haraka.

INAENDELEA UK.26

# Vilio vyatawala maziko

**Na Mwandishi Wetu**

VILIO, simanzi na majonzi vilitawala katika viwanja vya Shule ya Sekondari Morogoro na baadaye katika makaburi ya Kola Hill, baada ya miili ya waliofariki kwenye ajali hiyo kuzikwa.

Maelfu ya wananchi wa mkoa huo na jirani walijitokeza kuaga miili hiyo, huku Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiongoza waombolezaji.

Aidha, miili 69 ilizikwa yote na ndugu walijitokeza kupima vinasaba ili itakapotambulika kila kaburi litawekewa jina, lakini kwa jana ilizikwa na kupewa namba.

Wananchi 48 walijitokeza kutoa vinasaba kwa ajili ya utambuzi wa ndugu zao, na kwamba wapo ambao hawakuzikwa jana kwa kuwa ndugu waliomba kuzika wenyewe.

Mazishi hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali kuanzia ngazi ya taifa hadi wilaya, ikiwamo Wilaya ya Njombe ambako ndiko iliko Kampuni ya Chesco ambayo inamiliki gari lililolipuka na kuunguza idadi kubwa ya watu.

Mmoja wa ndugu wa marehemu, Omari Juma, alisema mtoto wa kaka yake alifariki na alikwenda Muhimbili kutambua katika majeruhi, lakini hakuona.

"Anaitwa Hassan Dachi hayumo katika majeruhi wala waliotambulika, lakini baada ya kupima vinasaba alitambulika na walikubali azikwe kwenye eneo hilo," alisema.

Aliwataka Watanzania kujifunza kutokana na tukio hilo wanaposikia mshtuko wasikimbilie, ikiwamo serikali kutoa elimu ya

INAENDELEA UK.26


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DODOMA
SHAURI LA ARDHI RUFAA NA. 17/2017

SUED AMANI LEMA ........................................MRUFANI

DHIDI YA

SAMSON NGUJI CHOMOLA NA WENZAKE ..................WAJIBU RUFAA

KWA:
1. SEMISTATUS HUSSEIN MASHAMBA
2. JALALA MUSTAFA YSUFU
3. GODFEY ROBERT SIMON
4. ISACK JOEL KUDEL
5. SALUM AWADH AL-GUHUM
6. MAPINDUZI ANDREA KIKASA
7. EMMANUEL LUSIANA DAFAY
8. SHAURI QAMANA
9. MWANZI YOHANES MBILINYI
10. ANNA LAWRANCE NGOWI
11. EDWARD ELIAS BUGANDA & ANNE ISDORY MSIKE
12. LILIAN JONARD KIMARO
13. IDDY SAI MAMBINA
14. PASCAL CHARLES MAGANDULA
15. RAPHAEL MAGALAMILE JOSHUA
16. ALPHA CHOLOBI

POPOTE PALE WALIPO

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA ARDHI RUFAA NA. 17/2017 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**MNAFAHAMISHWA KWAMBA;** shauri tajwa hapo juu linatajwa Mahakama kuu ya Tanzania,kanda ya Dodoma,mbele ya **MHE.JAJI L.MANSOOR,** wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3:00)kamili asubuhi siku ya ijumaa tarehe 23/8/2019.

**HIVYO;** Mnatakiwa mfike nyinyi wenyewe au Mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hamkufika nyinyi wenyewe au Mawakili wenu siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo nyinyi au Mawakili wenu kuwepo

**IMETOLEWA**; kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 29/07/2019.

215370002

# Aliyefungwa miaka 30 kwa madai kubaka aachiwa huru

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imetengua hukumu ya kifungo cha miaka 30 jela na kumwachia huru Saidi Hussein, kwa kosa la kubaka mwanafunzi wa darasa la saba baada ya kuona rufani yake ina mashiko ya kisheria ikiwamo umri wa mtoto anayedaiwa kumbaka kutokufahamika.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Dk. Atuganile Ngwala, mwishoni mwa wiki ilitengua hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya ya Temeke, kwamba ilikosea kumtia hatiani kwa sababu ushahidi wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha ushahidi wa kesi dhidi yake.

Katika uamuzi wake, Jaji alisema baada ya mlalamikaji kutiwa hatiani hakuridhika na adhabu hiyo na alikata rufani akiwa na sababu nane.

Mlalamikaji alidai sababu za rufani yake ni pamoja uchukuaji wa ushahidi wa mtoto haukufuata utaratibu, upande wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha kosa bila kuacha shaka, umri wa anayedaiwa kubakwa haueleweki na hakuna sababu za msingi za

INAENDELEA UK. 8



Wawakilishi wa Ujumbe wa SADC wakipata maelezo maalumu juu ya ubora wa malumalu zinazozalishwa na kiwanda cha KEDA kilichopo wilayani Chalinze, baada ya kuwasili kiwandani hapo kwa ziara ya siku moja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wiki ya pilikapilika Sadc

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUTANO wa 39 wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) unaendelea leo jijini Dar es Salaam ukiingia katika wiki ya pili na inatarajia kuwa Wiki ya Pilika pilika.

Mkutano huo ulioanza wiki iliyopita kwa Maonyesho ya Wiki ya Viwanda yaliyofunguliwa na Rais John Magufuli na kufungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein Alhamisi.

Leo mkutano huo unaendelea kwa kuwakutanisha makatibu wakuu wa idara, ambapo Mkurugenzi wa Miundombinu wa SADC, Mapoalao Mokoena, anatarajiwa kuzungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali.

Kesho, mkutano huo utaendelea kwa kuwakutanisha mawaziri wa SADC, kwa ajili ya kujadili mada mbalimbali ambazo baadaye zitawasilishwa kwa wakuu wa nchi za SADC.

Vilevile, wiki hii Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, anatarajiwa kupewa wadhifa wa kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri wa SADC.

Agosti 16, wakuu wa nchi za SADC wanatarajiwa kuanza kuwasilia nchini, pamoja na kufanyika kwa kikao cha Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC (TROIKA).

Kikao cha TROIKA kinatarajiwa kuwajumuisha Mwenyekiti wa sasa wa SADC ambaye ni Rais wa Namibia, Hage Geingob, Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Rais John Magufuli, na Mwenyekiti mstaafu wa SADC.

INAENDELEA UK. 8

## Sheria ya kuchangia viungo mbioni kutungwa

**Na Augusta Njoji, aliyekuwa** IRINGA

SERIKALI ipo kwenye mchakato wa kutengeneza sheria ya kuchangia viungo ikiwamo figo ili kusaidia wagonjwa wenye matatizo hayo.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Daktari wa Afya ya Akili kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ububuyu, alipokuwa akitoa mada ya magonjwa yasiyoambukiza kwa waandishi wa habari za usalama barabarani, mjini Iringa.

Alisema robo tatu ya wagonjwa wamekuwa wakikosa ndugu wa kuwachangia figo na wengine wakishindwa kumudu gharama za matibabu husuan kwenye kusafisha damu.

Dk. Ububuyu alisema kwasasa zinatumika taratibu na kanuni zingine za kuchangia, lakini inakuja sheria maalum itakayofanya suala hilo liwe kisheria.

"Ili kila mtu atakayechangia alindwe na sheria, kama mtu ataona hajafanyiwa kitu sahihi kwa sheria hiyo ataenda kwenye bodi maalum ambayo atapata haki zake," alisema.

Hata hivyo, alisema ugonjwa wa figo unatokana na sababu mbalimbali zinazotokana na magonjwa

INAENDELEA UK. 8

**Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-**

- **Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=**
- **Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=**
- **Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima**
- **Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku**

215227501



## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Global Packaging, Benno Mwitumba (kulia), akitoa maelezo juu ya utendaji kazi wa kampuni hiyo, inayotengeneza vifungashio bora nchini wakati wa ziara ya ujumbe wa mkutano wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) walipotembelea kiwanda hicho kilichopo Kibaha mkoani Pwani, kujionea ufanisi wa kiwanda na namna walivyojipanga kuingia katika soko la SADC.

# JPM alivyoing'arisha Takukuru Afrika

**Na Mary Geofrey**

TANZANIA imetajwa kuwa nchi ya kwanza kati ya nchi 35 za Afrika katika kipengele cha juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya rushwa kwa mwaka 2019, huku Rais John Magufuli akitajwa kuchangia mafanikio hayo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Diwani Athumani, alibainisha hayo mwishoni kwa wiki kwa wanahabari, akisema mafanikio hayo yametokana na juhudi za Rais Magufuli katika kupiga vita vitendo vya rushwa.

Alisema mafanikio hayo yameainishwa katika taarifa ya utafiti wa kupima hali ya rushwa, iliyotolewa Julai 11, mwaka huu na taasisi za kimataifa zinazofanya tafiti ambazo zimeainisha kuwa Tanzania imefanya vizuri katika maeneo mawili.

Alitaja maeneo iliyofanya vizuri ni utendaji mzuri wa viongozi wa serikali inayoongozwa na Rais Magufuli na kukuza imani ya wananchi dhidi ya serikali yao kutokana na jitihada za kuzuia na kupambana na rushwa nchini.

"Kumekuwa na ongezeko la idadi ya Watanzania wanaoamini kuwa serikali inafanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa kutoka idadi ya asilimia 37 mwaka 2015 hadi asilimia 71 mwaka 2019," alisema

INAENDELEA UK. 8

# Bunge laombwa sheria makosa yote dhamana

**Na Gwamaka Alipipi**

ZIKIWA zimepita siku kadhaa tangu mwandishi wa habari, Erick Kabendera kukamatwa, wadau wa habari na sheria nchini wametoa wito kwa Bunge kupitisha sheria itakayoruhusu makosa yote yawe na dhamana.

Wadau hao ni Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, Rais wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Deogratius Nsokolo na Makamu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile. Kwa pamoja wamesema mahakama ipewe mamlaka ya kutoa uamuzi kuhusu dhamana, masharti ya dhamana katika mahakama na Jeshi la Polisi yalegezwe ili kuweka masharti nafuu yatakayowawezesha watuhumiwa kupata haki yao.

"Makosa yote yawe na dhamana, sheria zote zinazominya haki ya watuhumiwa kupata dhamana zifanyiwe marekebisho ili kuwapa watuhumiwa haki yao ya kuwa huru wakati vyombo vya usalama vinapoendelea na uchunguzi au mahakama inapoendelea na kesi," alisema Nskolo.

Walisema mahakama inapaswa kupewa mamlaka ya kutoa uamuzi kuhusu dhamana, sheria zisizuie dhamana bali mahakama iamue kuhusu dhamana ya mtu kulingana na mazingira na uzito wa shauri.

Kadhalika, wadau hao walisema Jeshi la Polisi na vyombo vyote vinavyohusika na utoaji haki visikamate watuhumiwa kabla ya kumaliza upelelezi.

"Tunaungana na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma ya kuhakikisha watu hawakamatwi hadi pale uchunguzi wa kutosha uwe umefanyika, hii itapunguza muda mwingi wa watuhumiwa kukaa mahabusu," walisema wadau hao.

Walieleza kuwa sheria itakayotungwa itamke wazi kwamba ikifika kipindi fulani cha muda na upelelezi haujakamilika, kesi hiyo ifutwe. Walieleza kuwa kuwapo na utaratibu wa Jeshi la Polisi kupeleka shauri la kusikiliza ushahidi, hali hiyo itasaidia upatikanaji wa haki kwa wakati.

# Tuhuma za ubadhirifu zatumbua Bodi Shirecu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BODI ya Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Shinyanga (Shirecu), imevunjwa baada ya kudaiwa kufanya ubadhirifu wa shilingi 8,976,880, kinyume cha utaratibu wa matumizi ya fedha.

Bodi hiyo inadaiwa kuweka mhasibu mkuu hewa aliyelipwa Sh. 770,000 ndani ya siku kumi.

Bodi hiyo ilikuwa ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Richard Luhende; Makamu Mwenyekiti, Enock Lyela na wajumbe Donald Rogers, Dotto Kangoka na Jeremia Kapo.

Bodi hiyo ilivunjwa na Mrajisi Msaidizi wa Vyama vya Ushirika nchini, Josephat Kisamalala, alipokuwa anaongoza wa Mkutano Mkuu wa Shirecu, baada ya wajumbe 120 kupiga kura ya kuamua kuwakubali ama kuikataa bodi, hivyo kuikataa na Mrajisi huyo kutangaza kuitumbua. Kisamalala alisema bodi hiyo imevunjwa baada ya kubainika kufanya ubadhirifu wa kiasi hicho cha fedha na kuweka mhasibu mkuu hewa. Wajumbe 99 kati ya 21 walipiga kura za kuikataa bodi hiyo. "Bodi hii ya Shirecu imevunjwa rasmi, kwa sababu za kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha, na itaundwa nyingine, ambapo tutachagua majina ya watu saba ambao wataunda bodi mpya ambap ni waadilifu na waaminifu," alisema Kisamalala.

Naye Mkaguzi Mwandamizi wa Muungano wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Gabriel Msuya, alisema ukaguzi wa matumizi ya fedha kwenye katika Shirecu ulianza mwaka jana na kubainika kuwapo na ubadhirifu wa kiasi hicho cha fedha.

Naye Mwansheria kutoka Tume ya Maendeleo ya ushirika makao makuu, Donald Deogratius, alisema kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika, wajumbe wakiridhia bodi ivunjwe ina vunjwa, na kwamba wajumbe waliosababisha hasara chama wanapaswa kufidia fedha hizo. Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, alisema Shirecu sio taasisi ya mtu mmoja, hivyo serikali iliamua kufufua vyama vya msingi vya ushirika, ili kuwasaidia wakulima kunufaika na kilimo, na kwamba watakaofanya ubadhirifu, serikali haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria. Hata hivyo, Mwenyekiti wa bodi hiyo iliyovunjwa, Luhende, alikanusha kufanyika kwa ubadhirifu huo wa fedha, na kuikataa ripoti hiyo kwa madai hawakupewa nafasi ya kujieleza na imevunjwa kwa uonevu, huku makamu wake, Lyela akieleza kuridhika na maamuzi hayo.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga inawezekana zikijipanga dk. 90 za pili Caf

**MWISHONI** mwa wiki wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Simba, Yanga na KMC walilazimishwa sare katika mechi zao za awali kwenye Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba na Yanga zinapeperusha bendera ya nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati KMC na Azam FC ambayo jana ilikuwa dimbani dhidi ya Fasil Ketema ya Ethiopia, zinabeba jukumu hilo upande wa Kombe la Shirikisho.

Katika michuano hiyo inayoandaliwa na kuratibiwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), Simba ikiwa ugenini nchini Msumbiji ililazimishwa sare tasa dhidi ya UD Songo.

Na kwa upande wa Yanga ikiwa nyumbani katika Uwanja wa Taifa, ilibidi kusubiri hadi dakika ya 84 kuweza kusawazisha kwa mkwaju wa penalti kupitia kwa Patrick Sibomana wakati ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Township Rollers ya Botswana.

Miamba ya Kinondoni, KMC nayo ilitoka sare tasa ugenini nchini Kigali dhidi ya AS Kigali anayoichezea nyota wa zamani wa Yanga na Simba, Harouna Niyonzima.

Kwa ujumla matokeo hayo si mabaya sana kwa timu zote, ingawa kwa Yanga yanaweza kuwa si mazuri sana kwani kutokana na mfumo wa michuano hii inayochezwa nyumbani na ugenini kuruhusu bao la nyumbani linagharimu mechi ya marudiano.

Hata hivyo, kama ambavyo Kocha Mkuu wa Yanga Mwinyi Zahera alivyosema mara baada ya mechi kuwa timu yake inazidi kuimarika na anaweza kupata matokeo ugenini hata kwa kushinda 2-1, ndivyo ambavyo na sisi tunatamani kuona hilo likitokea.

Tunazidi kupata matumaini hayo, hasa kwa kuzingatia kauli ya Zahera kuwa hawana cha kupoteza wiki mbili zijazo ugenini na kwamba watakwenda kushambulia mwanzo mwisho, huku akiahidi kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza hususan katika safu ya ushambuliaji.

Lakini pia kwa upande wa Simba na KMC nazo hazipaswi kubweteka sana kwani matokeo ya sare tasa ugenini, yanahitaji umakini sana kwenye mechi ya marudiano nyumbani kwa kuhakikisha mgeni hapati bao. Hivyo, kwa ujumla kinachotakiwa kwa Simba na KMC na hata Azam, ni kuhakikisha zinatumia vema faida ya uwanja wa nyumbani mbele ya mashabiki wao.

Lakini pia, tunatambua kutopata matokeo kwa timu hizo kunaweza kuchangiwa na ukweli kwamba hizo ndizo mechi zao za kwanza za kimashindano msimu huu.


Na kwa namna zilivyoweza kucheza kwa kasi, hilo linatupa matumaini kwamba mechi zijazo za marudiano zitakuwa zimeimarika zaidi na kuweza kupata matokeo hususan kwa Yanga ambayo itakuwa ugenini.

Kinachotakiwa ni kutambua kuwa hizo ni dakika 90 za awali bado zingine kama hizo za kuweza kupata matokeo na kusonga raundi ya kwanza ya michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Nipashe tunaamini makocha wa timu zote zinazoipeperisha bendera ya nchi kwenye michuano hiyo wamebaini kilichowanyima ushindi na watakwenda kukifanyia kazi kabla ya marudiano na kuweza kusonga mbele.

Kuna wiki mbili za kujipanga upya kabla ya kurudiana mwezi huu kati ya Agosti 23-25, hivyo tunataka kuona timu zote nne zikisonga mbele na hilo litawezekana tu kama kutafanyika maandalizi ya kina, huku mashabiki wakiungana na timu zao dimbani kwa kuzishangilia mwanzo mwisho. Kila la heri wawakilishi wetu katika dakika 90 za pili Caf.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tanzanite wameweza Cosafa, serikali, TFF iwamulike zaidi

Na Adam Fungamwango

**IKIWA** ni timu alikwa kwenye michuano ya (COSAFA), Timu ya Taifa ya Tanzania ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20, imetwaa ubingwa na michuano hiyo kwa kuichapa timu ya Taifa ya Zambia mabao 2-1.

Michuano hiyo ilikuwa ikifanyika nchini Afrika Kusini, na mechi hiyo ya fainali ilichezwa jana Jumapili kwenye Uwanja wa Wilfson Port Elizabeth.

Chini ya Kocha Mkuu, Bakari Shime, mabao ya Tanzanite yalifungwa na Opa Clement dakika ya 24 na Protasia Mbunda dakika tatu kabla ya pambano kumalizika.

Ilikuwa ni hoi hoi nderemo na vifijo kwa kinadada hao wa Kitanzania mara baada ya filimbi ya mwisho ya mechi hiyo, huku wakipewa sapoti na baadhi ya Watanzania wanaoishi nchini humo, waliokuwa wakishangilia kwa nguvu, wakiwa wamebeba bendera ya Tanzania.

Uchezaji na nyimbo za Kibongo zilizokuwa zikiimbwa na kinadada hao, benchi la ufundi pamoja na Wabongo waishio Sauzi vilikuwa ni burudani tosha.

Pongezi kubwa kwa kocha mkuu, viongozi walioandamana na timu hiyo, wachezaji pamoja Shirikisho la Soka nchini (TFF) na Watanzania wote kwa ujumla.

Kwa mara nyingine tena imedhihirisha kuwa kwa sasa Tanzania imeanza tena kuanza kupiga hatua kwenye masuala ya michezo.

Miaka kadhaa nyuma, Tanzania haikuwa na chochote cha kujivunia kwenye nyanja za michezo kiasi cha hata Wabongo kushindwa kutamba wanapokwenda kwenye nchi zingine.

Tangu Hassan Mwakinyo alipoanza kumchapa bondia mzungu nchini Uingereza, Simba kufika robo fainali Ligi ya Mabingwa, Taifa Stars kufanikiwa kufuzu AFCON kwa mara ya kwanza baada ya miaka 40, pamoja na ushindi wa majuzi wa Taifa Stars wa kutafuta kufuzu CHAN, nchi imekuwa na maendeleo mazuri na hata mwelekeo umeanza kuonekana kuwa mzuri.

**Hata Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliliongelea hilo kwenye tamasha la Simba Day, lakini pia akitamka kuwa serikali imeruhusu uwekezaji kwenye klabu kwa ajili ya kuzifanya kuwa nzuri kiuchumi na kuzidi kufanya vema kimataifa na kuiletea sifa nchi.**

Hata Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliliongelea hilo kwenye tamasha la Simba Day, lakini pia akitamka kuwa serikali imeruhusu uwekezaji kwenye klabu kwa ajili ya kuzifanya kuwa nzuri kiuchumi na kuzidi kufanya vema kimataifa na kuiletea sifa nchi. Pamoja na pongezi, lakini kinachotakiwa sasa ni kutojisahau kwani kinadada hao ndiyo wanaokwenda baadaye kuunda kikosi cha timu ya Taifa ya Wanawake, Twiga Stars hivyo inafaa waangaliwe kwa jicho pana zaidi.

Tatizo kubwa ninaloliona kwenye timu za vijana za wanaume na wanawake Tanzania, huwa na wachezaji wenye vipaji, lakini wengi hupotelea kati na huwa hawajulikani wanapoenda.

Watanzania tusipende tu kuwapokea kwa kishindo na mbwembwe nyingi wanapokuwa wanamichezo wameshinda na baada ya hapo wanaachwa waendelee na maisha yao, hapo ndipo tunapowapoteza.

Uchunguzi mdogo unaonyesha kuwa wengi wao wanashindwa kuendelea na vipaji vyao kutokana na wazazi wao kuwataka wakazanie zaidi masomo kuliko michezo, wengine wanaachana na soka na kuanza kusaka pesa kwa sababu ya matatizo ya kifamilia na wengine wanalewa sifa na kushindwa kujitambua na kujitunza hadi kudumaza vipaji vyenyewe.

Kwa kinadada hawa, inabidi TFF na serikali kupitia wizara husika kukaa chini na kufanya mikakati ya kuwasaidia mabingwa hawa ili kulinda vipaji vyao visaidie taifa mbele ya safari kama vilivyofanya huko Sauzi.

Kwanza kabisa wawe wanakutana mara kwa mara kwa ajili ya mazoezi, lakini pia kuwasaidia kwenye masomo yao kama vile ada na mambo mengine ambayo familia zao zinashindwa kutatua, na kupewa ushauri nasaha ni jinsi gani ya kujitambua na kujitunza ili kuepuka kufifisha vipaji vyao.

BARUA & MJADALA

## Hii serikali imetuvusha

**Mhariri,**

*NIANZE kutamka faraja yangu namna serikali ya awamu ya tano ilivyo macho na mstari wa mbele katika kujikweza na kuwajibika kwa dhati katika tafsiri kamili ya maendeleo.*

*Tukisimamia ukweli, sote tutaangukia katika ushuhuda wa shughuli za ukarabati na ujenzi wa majengo na miundombinu mingi kama vile barabara, shule, hospitali na miradi ya upanuzi wa huduma za umeme kitaifa. Nitumie msamiati "mwenye macho haambiwi tazama."*

*Binfasi, bila ya kuweka ushabiki wa kisiasa, niseme Rais Dk. John Magufuli, anatimiza alichokiahidi wakati wa kampeni. Katika hicho niseme jambo bayana kuwa ni binadamu anayependa kuingia katika mabadiliko ya kusonga mbele katika maisha ya wananchi wake.*

*Kadri siku zinavyosonga mbele, tunazidi kuwa mashuhuda wa miradi mikubwa inayogharimiwa na fedha kutoka kodi za wananchi. Hapo nisifu namna inavyoainishwa matunda ya kodi ya wananchi na kile kinachojitokeza kutetea maendeleo yao.*

*Pia, katika eneo hilo niseme namna ilivyoanzishwa kodi ya shilingi 20,000 kila mwaka na ilivyofungua mlango mpana wa uhuru wa kikazi kewa wajasiriamaili na fursa ya kusonga mbele, inapaswa kuingia katika historia kuu ya maendeleo kitaifa.*

*Hiyo inatokana na ukweli bayana wa namna wajasiriamali wadogo na walioko mitaani, pia wasio na vituo maalumu au vya kudumu kuendesha kazi zao maarufu kama 'Machinga' walitapatapa kwa madhila mengi ikiwamo kukimbizwa na mgambo na kunyang'anywa bidhaa zao, sasa wanapumua kufurahia uhuru mpya wa kudumu.*


*Ni uhuru unaosimamiwa na agizo la kisheria kutoka kwa mkuu wa nchi, tena kwa gharama ndogo ya kodi kwa mwaka ambayo inaangukia wastani wa shilingi 55 tu kwa siku.*

*Nimbatize kuwa 'jembe lenye makali.' Hivyo, ni jukumu letu kumuunga mkono kuelekea matokeo chanya zaidi.*

**Mtunzi wa Vitabu,**
**Joseph Yesaya Msindai,**
**Dar es Salaam,**
**Simu: 0712946671**

**WASILIANA NASI:**
TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU
mhariri@nipashe.co.tz

# KMC inaweza kushangaza wengi kimataifa




**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA shabiki yeyote aliyeamini kama timu ya KMC ingeweza kwenda kuvimba na kulazimisha sare ya bila kufungana dhidi ya AS Kigali ya nchini Rwanda kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (Caf).

Kwa sababu ni timu ambayo bado changa kwenye Ligi Kuu, ikiwa imecheza msimu mmoja tu, utakaofuata utakuwa ni wa pili kwao. Ilipata bahati ya kucheza mechi za kimataifa baada ya Caf kuiongezea Tanzania timu za kushiriki michuano hiyo kutoka mbili hadi nne kufuatia Simba kufika robo fainali msimu uliopita.

KMC ilishika nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu msimu uliopita na imepata nafasi hiyo baada ya Azam iliyotakiwa kucheza michuano hiyo baada ya kushika nafasi ya tatu, kuwa ndiyo bingwa wa Kombe la FA, hivyo nafasi hiyo ikaenda kwa timu hiyo changa.

Pamoja na uchanga wake, timu hiyo inaonekana kuwa na viongozi makini kwani baada ya kupata nafasi hiyo waliamua kuongeza wachezaji ambao wana uzoefu na michuano hiyo, baadhi yao kama Janvier Bokungu, mchezaji wa zamani wa TP Mazembe, Esperance na Simba.

Huyo pamoja na wengine wamekifanya kikosi hicho kutoka kuwa KMC ya kawaida na kuwa moja ya timu tishio Afrika Mashariki na Kati kwa muda mfupi tu.

Kukubali kwenda kushiriki michuano ya Kombe la Kagame kwa kiasi kikubwa ndiko kulikoifungua macho timu hiyo na kupata uzoefu kiasi cha kuweza kupata hata hiyo sare ya ugenini.

Kama itashinda na kwenda hatua inayofuata, KMC inaweza kuendelea kufanya vema kimataifa na kuendelea kuwashangaza wengi.

Ni timu ambayo mpaka sasa bado wapo watu wachache wanaoona kama inabahatisha, lakini kuna siku watakuja kukubali kuwa viongozi na klabu hiyo, benchi la ufundi na wachezaji wamejipanga.

Kama ikiangaliwa vizuri na kusiwapo mgogoro wowote ule, KMC inaweza kuwa ni zaidi ya Azam FC na kuleta mageuzi ya hali ya juu kwenye soka la Tanzania.

Azam iliyopanda msimu wa 2008, imekuwa ndiyo timu pekee mpaka sasa ambayo inazitia homa Klabu za Simba na Yanga si tu inapokutana nazo, lakini pia hata lengo la matarajio ya klabu hiyo.

Ukiangalia kiuhalisia ni kwamba klabu tatu tu za Simba, Yanga na Azam ndizo zinazoanza Ligi Kuu zikihitaji ubingwa, huku zilizobaki zikionekana kabisa kwa vitendo kuwa zinadunduliza pointi za kuzibakisha zisishuke tu.

Hali hii inasababisha Ligi Kuu Tanzania Bara isiwe na ushindani unaotakiwa na kufanya iwe na matabaka tangu mwanzo.

Ligi yoyote imara huwa inagawanyika ikikaribia mwisho, lakini mwanzoni timu zinafukuzana, hii ni tofauti na Tanzania ambako tangu mwanzo tu timu hizo tatu ndiyo zinaonekana kukimbizana.

Na hata KMC kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa ni sababu ya Mtibwa Sugar na Lipuli kuona zimemaliza baada ya kuwa na pointi ambazo haziwezi kushuka daraja zikaanza kufanya vibaya.

Kwa muda mrefu zilikuwa zinapokezana nafasi ya nne, lakini ziliona kama inatosha na kuifanya KMC iliyokuwa katikati ya misimamo kuwafikia na kuwapita hadi kushika nafasi ya nne.

Ni kwa sababu hawakujua kama nafasi hiyo kwa sasa ni dili, laiti kama timu hizo zingejua, sidhani kama KMC ingewakilisha nchi.

Lakini KMC tangu mwanzo, pamoja na upya wake, haikucheza ligi kwa kukusanya pointi ili ibaki Ligi Kuu bali ni kupambana mwanzo hadi mwisho wa ligi na kuangalia itakapofikia.

Kama imefanya hivyo kwa mara ya kwanza, basi timu hiyo itakuwa inaongeza timu ambazo zitakuwa zikisaka ubingwa tangu mwanzo wa ligi.

KMC inaweza kuwa timu tishio zaidi si kwa Simba na Yanga tu bali pia Azam ambayo kwa miaka ya karibuni si imara kama ile ya miaka mitatu ama minne iliyopita.

Na kwa usajili ilioufanya, KMC na umakini wao, wanaweza kabisa kuvaa viatu vya Azam na kufanya vema kimataifa kama timu hiyo ilivyofanya miaka kadhaa iliyopita, ingawa ilikuwa ikitolewa kwenye hatua zinazofuata.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Sheria ya kuchangia viungo mbioni kutungwa

INATOKA UK. 4

yasiyoambukiza kama vile kisukari, moyo na shinikizo la damu. Alibainisha kuwa wagonjwa ambao wamesajiliwa kutokana na figo kutofanya kazi nchini kwa sasa ni takriban 851 kwenye hospitali za kanda, rufani na taifa.

"Hawa wanahitaji huduma ya figo bandia, wanahitaji mashine iwasaidie kusafisha damu au kupandikizwa figo, na gharama za matibabu yake ni kubwa hasa katika kusafisha damu," alisema.

Aliongeza kuwa: "Kwa session moja mgonjwa wa kusafishwa damu itamgharimu mtu Sh. 250,000 hadi Sh. 300,000 na anatakiwa awe na session tatu kwa wiki moja, hivyo ndani ya mwezi Sh. milioni 3-4, hata uwe Gavana wa BoT ni ghali sana."

Alisema kwa mwaka mgonjwa atalazimika kutumia Sh. milioni 36-48, na kama kisukari na shinikizo la damu vitaendelea kushambulia itasababisha figo kushindwa kufanya kazi.

Mtaalamu huyo alisema takriban Sh. bilioni 26 hadi 40 zinahitajika kwa mwaka kwa wagonjwa wa figo kwa ajili ya kusafishwa damu na asilimia 30 ya wagonjwa wanashindwa kumudu gharama hizo na serikali inalazimika kubeba mzigo.

"Hizo gharama ni kubwa hata zikiingizwa kwenye bima kwa asilimia 100 itahatarisha mfuko, ni changamoto, mpaka sasa wagonjwa 40 wamepandikizwa, tuhamasishe wananchi kuchangia figo," alisema.

Kwa magonjwa yasiyoambukiza, alisema yanaendelea kuongezeka nchini na kuchangia vifo kwa asilimia 33.

"Pia takwimu za kidunia zilizotolewa na WHO, magonjwa yasiyoambukiza yanaongoza kwa kuua watu wengi zaidi mpaka sasa takwimu zinaonyesha kwamba kwa mwaka 2012 watu milioni 16 wamefariki dunia kutokana na vifo visivyotarajiwa. "Vifo visivyotarajiwa ni vile vya kabla ya miaka 70 na asilimia 82 ya vifo hivyo vimetokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema.

Alibainisha kuwa upatikanaji wa dawa ni changamoto na dawa zake ni za gharama kubwa na mzigo kwa serikali na kwa watu binafsi.

"Watu wengi wanachelewa kupata tiba ya magonjwa kama vile sukari, moyo au saratani kutokana na kuchukua muda mrefu kugundulika," alisema.

Vile vile, alisema katika utafiti uliofanywa na Stepwise Surveillance (STEPPS) Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani ulioshirikisha Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Wizara ya Afya kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, asilimia 25 ya waliopimwa wana changamoto ya shinikizo la juu la damu na kwa bahati mbaya asilimia 68 ya watu hawakuwahi kujua kabla kuwa wanaumwa.

"Katika kila watu wawili kati ya watatu hawajui kama wana tatizo la shinikizo la damu, magonjwa mengine kama selimundu,

Tanzania inaingia katika nchi 10 duniani zenye tatizo hilo, na kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa sita wana tatizo la selimundu," alisema. Alifafanua kuwa vipo vihatarishi vingi vya magonjwa hayo ikiwamo lishe duni kwa kula chakula ambacho hakipo kwenye mpangilio unaotakiwa, uzito uliopitiliza, mtindo wa maisha ikiwamo kubweteka kutoshughulisha mwili.

"Vingine ni vilevi hata mwanamke kipindi cha ujauzito hatakiwi kutumia pombe kabisa kwa kuwa anamuweka mtoto kwenye hatari katika ukuaji wake," alisema.

### MIKAKATI YA SERIKALI

Alisema magonjwa hayo kutokana na kuwa na gharama kubwa serikali inajipanga kutengeneza mpango maalum wa kudhibiti na kuzuia magonjwa hayo.

"Pia tutakuwa na wiki ya magonjwa yasiyoambukiza tuunganishe nguvu zote kukabiliana nayo, kutakuwa na kampeni maalum kama ilivyofanyika kwa magonjwa mengine, itafanyika Novemba 9 hadi 16 na mwaka huu itafanyika Dodoma," alisema.

# JPM alivyoing'arisha Takukuru Afrika

INATOKA UK. 5

Alisema pia utafiti unaonyesha kuwa idadi ya wananchi wanaofikiri kuwa rushwa imeongezeka nchini ni ndogo kwa asilimia 10, ikilinganishwa na idadi ya asilimia 66 iliyoona hivyo mwaka 2015.

Alisema utafiti huo pia umeonyesha kuwa idadi kubwa ya Watanzania wana imani na serikali yao juu ya mapambano dhidi ya rushwa na wanaona vitendo hivyo vimepungua. Imani imeongezeka kutoka asilimia 13 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 72 kwa mwaka 2019. "Moja ya sababu kubwa ya mafanikio haya ni utashi wa kisiasa aliyonayo Rais wetu Magufuli, katika kuongoza mapambano haya kutokana na imani ya wananchi kwa serikali kuongezeka, nidhamu ya watumishi serikalini imeimarisha na vilevile matumizi mabovu ya fedha ndani ya serikali yamepungua," alisema Diwani.

Aliahidi kuwa wataendelea kufanya kazi vizuri katika mapambano hayo na kuwataka Watanzania kuwa mstari wa mbele kuunga mkono jitihada hizo.

### ONYO WIMBI LA MATAPELI

Katika hatua nyingine, bosi huyo wa Takukuru alisema taasisi hiyo kumezuka wimbi la matapeli wanaojifanya kuwa maofisa wa Takukuru pamoja na baadhi ya vyombo vya ulinzi na usalama nchini wanaowatapeli watu.

Diwani alisema wanaokaidi kutoa hongo hiyo hutishiwa kuwaelekeza kuripoti katika ofisi za taasisi hiyo makao makuu na mikoani. Alisema matapeli hao wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali ikiwamo kuwapigia simu wananchi wakiwataka wawape hongo ili wasichukuliwe hatua kwa madai kuwa wanatuhumiwa kwa makosa ya rushwa. "Kupitia taarifa hii ninatoa onyo kali kwa wale wote wanaotaka kuchafua taswira chanya ya Takukuru pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, kuacha mara moja tabia hiyo yenye lengo la kuondoa imani ya wananchi kwa serikali yao," alisema Diwani.

Aliwataka wananchi kutokubali kudanganywa na yeyote bila kumdadisi japo kumtaka ajitambulishe na ikiwezekana atoe kitambulisho na kueleza kosa kwa sababu ni haki ya kila mwananchi.

"Napenda kuusisitizia umma kwamba Takukuru haifanyi kazi zake vichochorini, ofisa wa Takukuru hufanya kazi zake za kiuchunguzi akiwa na kitambulisho pamoja na nyaraka halisi zinazompa mamlaka ya kufanya uchunguzi wake nje ya ofisi," alisema.

Alieleza zaidi kuwa watu ambao wamekuwa wakitaka kutapeliwa wamekuwa wakielekezwa kufika katika ofisi hizo ndipo wanatambua kuwa waliofanya vitendo hivyo ni matapeli.

Alifafanua zaidi kuwa ofisa wa Takukuru hufanya mahojiano katika ofisi zake zilizopo kila mkoa na wilaya, na kuwa wananchi wawe makini kuwadadisi na kuwahoji wanaotaka kuwatapeli.

"Pia kwa yoyote atakayemtilia shaka anayejitambulisha kwake kama ofisa wa Takukuru, awasiliane nasi kwa kupiga simu bure kwenda namna 113 au kutuma ujumbe mfupi kupitia namba hiyo hiyo nasi tutashughulikia," alisema.

# Aliyefungwa miaka 30 kwa madai kubaka aachiwa huru

INATOKA UK. 4

kumtia hatiani.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi wanne akiwamo msichana anayedaiwa kubakwa, mlalamikaji alikuwa akiishi Tuangoma, mwanafunzi alikuwa akisoma darasa la saba mwaka 2016.

Ilidaiwa kuwa mwanafunzi huyo Machi, 2016 alikuwa akiuza ndoo akakutana na mrufani akaomba amuuzie ndoo kwa Sh. 1000, lakini alikataa.

Ilidaiwa kuwa Desemba 2016 akiwa maeneo ya shuleni mwanafunzi huyo alikutana na mlalamikaji akamwambia kwanini anamkataa, leo (siku ya tukio) akikataa atamuua au kumchuna ngozi, akamchukua na kumpeleka katika nyumba ambayo haijaisha na kufanya naye mapenzi.

Ilidaiwa baada ya tendo hilo mlalamikaji alimpa Sh.5,000, lakini waliendelea kukutana katika nyumba hiyo na kufanya mapenzi, maendeleo darasani yakaanza kushuka, kaka yake akashtuka ndipo alipoanza kumfuatilia dada yake, alipombana alieleza badala ya kwenda shule huwa anakwenda kufanya mapenzi katika nyumba hiyo.

Ilidaiwa kuwa kaka wa mwanafunzi huyo alitoa taarifa shuleni, mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa mahakamani, daktari alithibitisha kwamba aliingiliwa na kitu butu, hakimu aliridhishwa kwamba mtuhumiwa ndiye alifanya hivyo akamtia hatiani.

"Mahakama yangu imepitia ushahidi uliotolewa katika kesi ya msingi na kwamba ina maoni tofauti kwa kuzingatia msingi na kanuni zilizowekwa, kabla ya kuchukua ushahidi wa mtoto lazima maswali matatu yaulizwe na hakimu au jaji kwa mtoto, lakini kumbukumbu zinaonyesha hakimu hakufanya uchunguzi kabla ya kuchukua ushahidi wa mwanafunzi huyo," alisema na kuongeza:

"Ushahidi wa Jamhuri unatofautiana na kwamba hata hakimu hakuchunguza umri wa mtoto, hakuna kinachoeleza kuhusu umri halisi wa mwanafunzi huyo, kuna shahidi anasema alikuwa na miaka 13, mwingine 15 na hati ya mashtaka inasema alikuwa na miaka saba," alisema Jaji Dk. Ngwala.

Pia alisema kwa kupitia ushahidi wote hakuna kielelezo kilichotolewa kuthibitisha umri wa mwanafunzi huyo, kwa mazingira hayo mahakama inashindwa kuona aliyebakwa alikuwa mtoto au ni mtu wa umri gani.

Alisema mahakama yake imeona rufani ya mlalamikaji ina mashiko ya kisheria inamwachia huru dhidi ya adhabu hiyo ya miaka 30.

# Wiki ya pilikapilika Sadc

INATOKA UK. 4

Katika kikao hicho, wakuu wao watajadili masuala ya amani, ulinzi na usalama kuhusu nchi za SADC.

Agosti 17 hadi 18 mkutano mkuu wa wakuu wa nchi za SADC utafanyia.

**Wakati huo huo**, nchi za SADC zipo katika mchakato wa kuunda Mfuko wa Kilimo wa Kanda ambao utakuwa na lengo la kuzisaidia nchi wanachama kuinua sekta hiyo.

Mfuko huo pia utakuwa na lengo la kupambana na mabadiliko ya tabianchi, wadudu vamizi wa mazao ya kilimo, ambao wamekuwa kikwazo katika kuinua sekta ya kilimo katika nchi nyingi za SADC.

Mkurugenzi wa Idara ya Chakula, Kilimo na Maliasili (FANR) wa SADC, Domingo's Gove, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mipango ya baadaye ya idara hiyo.

"Sekta ya kilimo ni muhimu katika kuchochea maendeleo na uchumi wa nchi 16 za SADC, hivyo ni wakati muafaka wa kuja na mfuko huo, sekta ya kilimo inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama mabadiliko ya tabianchi, wadudu vamizi kama viwavijeshi na njia ya kukabiliana navyo ni kuwapo na chombo rasmi kwa ajili hiyo," alisema Gove na kuongeza:

"Katika kuhakikisha sekta ya kilimo inakuwa na tija kwa nchi wanachama, tupo kwenye mchakato wa kuja na mfuko wa kilimo ambao utasaidia nchi zote," alisema Gove.

Alisema kuna mbegu zaidi ya 48 katika nchi wanachama wa SADC ambazo wanazipa kipaumbele kulingana na mazingira ya nchi husika.

Gove alisema mfuko huo utasaidia upatikanaji wa mbegu bora, mbolea, dawa na kusaidia kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima miongoni mwa nchi za SADC, na kwamba iwapo kila nchi itashiriki kikamilifu ni dhahiri sekta hiyo itachangia uchumi na maendeleo kwa kasi.

"Mkakati wetu ni kuwa na mbegu ambazo hazishambuliwi na wadudu vamizi kama viwavijeshi, zaidi ya 48 katika nchi wanachama za SADC ambazo wanazipa kipaumbele kulingana na jiografia ya nchi husika," alisema Gove.

Alifafanua kuwa mfumo huo utasaidia utekelezaji wa vipaumbele vinne vya SADC katika sekta hiyo muhimu ambavyo ni kukuza uzalishaji na ushindani katika sekta.

Alisema idara hiyo imejipanga kutafuta na kutangaza masoko, kuhamasisha sekta binafsi katika uwekezaji na kuongeza usalama wa chakula.

Gove alisema mipango na mikakati ambayo inatekelezwa na SADC itakuwa na tija iwapo itashabihiana na sera za nchi wanachama katika sekta husika.

"Sekta ya kilimo inaweza kuleta mapinduzi iwapo itashabihiana na uwapo wa viwanda, miundombinu, ulinzi na usalama na programu maalum na Tanzania imeonyesha mfano," alisema.

Kwa upande mwingine Gove amezikumbusha nchi za SADC kutekeleza azimio walilokubaliana viongozi kwa kutenga asilimia 10 katika bajeti za nchi kuelekezwa kilimo.

Alisema sekta hiyo ikipewa kipaumbele nchi na wananchi watafanikiwa kiuchumi na maendeleo.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akizungumza na wachimbaji wadogo katika eneo la Mataba ndani ya shamba la miti la Biharamulo- Chato linalisimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuhusu umuhimu wa kufuata sheria na taratibu za kuchimba madini ndani ya hifadhi mkoani Geita. **PICHA: WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

# NEMC yaagizwa udhibiti chuma chakavu mipakani

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira),

George Simbachawene, ameli-taka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kutumia ofisi zake za kanda kudhibiti usafirishwaji wa chuma chakavu maeneo yote ya mipaka.

Akizungumza mwishoni mwa wiki mara baada ya kuhitimisha ziara yake ya

= siku moja ya kutembelea Bandari ya Dar es Salaam kujionea namna zoezi la usafirishaji wa chuma chakavu inavyoendeshwa, Waziri Simbachawene hakuridhishwa na utaratibu unaotumika sasa kusafirisha chuma chakavu kwani unachangia upotevu wa mapato ya serikali.

"Biashara hii inafaida kubwa kwa wafanyabiashara na utaratibu unaotumika sasa kusafirisha chuma chakavu hauisaidii serikali kupata mapato kupitia kodi kwa kuwa hakuna utaratibu wa kutoa risiti," alisema Simbachawene.

Waziri alisema katika kipindi hiki ambapo azma ya serikali ni kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025, chuma chakavu ni moja ya malighafi muhimu zaidi kwa viwanda vya nchini.

Simbachawene pia aliwataka Wakuu wa Mikoa na Wilaya kusaidia kudhibiti usafirishaji

wa chuma chakavu katika maeneo yao na hasa mipakani ili kuzuia upotevu wa mapato ya serikali.

Aidha, waziri ametoa muda kwa mamlaka husika kutoa maelezo ya kina juu ya makontena 18 ya chuma chakavu iliyosafirishwa nje ya nchi licha ya kuwepo kwa zuio la kusafirishwa makontena hayo.

"Mamlaka zote zinazohusika na ukaguzi wa chuma chakavu kabla havijasafirishwa zikae pamoja na zije na majibu ya kwa nini makontena,18 yamesafirishwa licha ya kuwapo na zuio la kutosafirishwa, chuma chakavu ni biashara kubwa sasa pengine kuliko hata madini," alisisitiza Simbachawene.

Meneja wa Forodha Bandari ya Dar es Salaam, Njaule Mdendu, alisema kuwa ziara ya waziri imetoa mwanga mpya katika kusimamia usafirishaji wa chuma chakavu na kuahidi kufanyia kazi changamoto zake.

"Tunamshukuru waziri kwa namna alivyotoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo hali ambayo itaongeza ufanisi, lakini hata hivyo uwapo wa maofisa wakazi wa NEMC unaweza kusaidia katika kutoa elimu na kufanya ukaguzi wa chuma gani inapaswa kubaki na vipi vinapaswa kusafirishwa nje ya nchi badala ya kuja na kuondoka," alisema Mdendu.

# Makonda aichachamalia Kinondoni

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameutaka uongozi wa Manispaa ya Kinondoni, kuhakikisha unaanza ujenzi wa maboresho ya fukwe za Coco ndani ya mwezi mmoja vinginevyo atawanyang'anya fedha na kumtafuta mzabuni.

Ni miezi mitano imepita tangu serikali itoe fedha hizo lakini utekelezaji wa mradi huo wa Sh. bilioni 14 haujaanza. Makonda alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipotembelea fukwe hizo kwa lengo la kuangalia maendeleo ya mradi huo, lakini alishangazwa kuona hakuna kazi inayoendelea. Alisema watendaji wamekuwa wakilumbana wakati fedha za mradi huo zikiwa benki bila matumizi yoyote.

"Kinachosikitisha zaidi ni kuona mshauri wa mradi amebadili mchoro wa mwonekano mpya wa fukwe ambao ndio ulioombewa Sh. bilioni 14 na kuja na mchoro wake mwingine wa Sh. bilioni 40 bila kujua fedha hizo zitatoka wapi, hii ni hujuma kwa serikali," alisema Makonda.

Alisema wananchi wanapaswa kutambua kuwa mradi huo unacheleweshwa kwa uzembe wa watendaji wachache wanaoshinda kwenye vikao visivyomalizika.

Aidha, Makonda alizitaka halmashauri zote mkoani humo kuhakikisha fedha zinazotolewa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi zinatumika kwa lengo husika na siyo kuwekwa kwenye akaunti.

Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa Sh. bilioni 28 kwa wilaya hiyo kwa ajili ya kuendeleza miradi miwili ya ujenzi wa soko la Tandale na uboreshaji kwa kuendeleza ufukwe wa Oysterbay, maarufu Coco Beach, lengo likiwa ni kulipa thamani eneo hilo na kuongeza watalii wa ndani na nje ya nchi. Utiaji saini kwa ajili ya mkataba wa ujenzi huo, ulifanywa Februari 4 mwaka huu kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dotto James na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Aron Kagulumjuli.

# TFS ilivyotumia maonyesho SADC kutangaza utalii

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), imesema kupitia Maonyesho ya Nne ya Viwanda kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), imepata nafasi ya kueleza fursa mbalimbali zinazopatikana kama kutangaza utalii.

Meneja Masoko wa TFS, Mariam Kobero, alisema kupitia maonyesho hayo ambapo washiriki kutoka nchi mbalimbali walielimishwa namna TFS inavyotekeleza majukumu yake kwa niaba ya serikali hususan uhifadhi wa misitu asilia na ufugaji nyuki na mazao yake.

"Kipindi chote cha maonyesho ya SADC, tumekuwa tukitoa elimu kuhusu TFS na majukumu yake na sehemu kubwa ya waliotembelea banda letu walionekana kutaka kufahamu zaidi kuhusu ufugaji nyuki kibiashara, wengine walieleza wanavyovutiwa na ubora wa asali ya Tanzania," alisema Kobelo na kuongeza:

"Hata hivyo katika eneo la asali pamoja na mambo mengine, tumekuwa tukiwaeleza kuwa ili kuhifadhi vizuri asali kwenye chupa siyo lazima kuwa na mtambo mkubwa bali unaweza kuwa hata na mtambo mdogo na ukapata asali ya kutosha."

Kuhusu utalii unaotokana na uhifadhi wa misitu asilia, Kobero alisema TFS iliona haja ya kutumia nafasi hiyo kuelezea aina hiyo ya utalii kwa nchi za SADC na lengo ni kuwaambia kuwa Tanzania kuna utalii ikolojia, hivyo ni vyema wakafika kwenye misitu iliyopo nchini ambapo kwa sasa kuna misitu asilia 17.

"Ikolojia ni eneo zuri kwa utalii, hivyo tunazihamasisha nchi za SADC kuja kuwekeza kwenye utalii huo na wakati huo huo tunawahamasisha wafike kwenye vivutio hivyo ambavyo mazingira ya misitu ni tulivu na ndani yake kuna utalii wa kila aina," alisema Kobero.

# NMB yasaidia shule, vituo afya mil. 50/-

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NMB imetoa msaada wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya kusaidia sekta za afya na elimu katika wilaya za Musoma na Butiama mkoani Mara.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Agustino Abraham, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kutaka kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha huduma za kijamii hususan katika sekta ya elimu na afya.

Alisema benki yake imeamua kusaidia sekta hizo hasa ikizingatiwa kuwa serikali ina sera ya uchumi wa viwanda na sera hiyo haiwezi kufanikiwa endapo sekta za afya na elimu hazitakuwa imara.

Alisema kutokana na umuhimu wa sekta hizo katika ukuaji wa uchumi wa taifa na jamii kwa ujumla benki yake imekwisha tumia zaidi ya Sh. milioni 550 kuboresha sekta hizo nchini kati ya Sh. bilioni moja ambazo zimetengwa na NMB kwa ajili ya kutoa msaada katika sekta hizo mwaka huu.

Alisema msaada uliokabidhiwa ni pamoja na madawati, vitanda kwa ajili ya wagonjwa na vingine kwa ajili ya kinamama kujifungulia pamoja na mabati, huku akisema kuwa msaada huo itanufaisha shule tatu za msingi na tatu za sekondari pamoja na vituo vitatu vya afya katika wilaya za Musoma na Butiama.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, aliishukuru benki hiyo ambapo alisema serikali imepanga kuboresha sekta za afya na elimu, lakini juhudi hizi zinahitaji ushirikiano kutoka kwa wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za kifedha.

Malima alisema pamoja na kupokea msaada huo lakini serikali mkoani Mara bado inahitaji msaada na ushirikiano mkubwa kutoka kwa benki hiyo ili kuweza kuboresha mazingira ya elimu hususan kwa watoto wa kike.

Alisema kuwa kutokana na mkoa wa Mara kuwa miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa vitendo vya ukatili, serikali imepanga kujenga makambi maalum maarufu kwa jina la nyumba salama kwa ajili ya kuwahifadhi watoto wa kike ili waweze kuepukana na vitendo vya ukatili ambavyo kwa namna moja ama nyingine vimekuwa vikisababisha watoto wengi wa kike kuacha masomo na hivyo kushindwa kutimiza ndoto zao za elimu.

Akizungumza kwa niaba ya walimu walionufaika na msaada huo, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Buhare iliyopo Manispaa ya Musoma, Jonas Zakayo, alishukuru NMB kwa msaada huo ambao alisema kuwa utasaidia katika kuboresha elimu na taaluma katika shule hizo.

# Kinamama walilia vifaa kituo cha afya

**Na Lilian Lugakingira,**
MULEBA

BAADHI ya kinamama ambao wanategemea kupata huduma za afya katika Kituo cha Afya Izigo wilayani Muleba mkoani Kagera, wameiomba serikali kuwezesha upatikanaji haraka wa vifaa katika jengo jipya la huduma ya mama na mtoto ili lianze kutumika.

Wamesema lilianza kutumika litawapunguzia adha wajawazito na waliojifungua kulazwa kwa kuchanganywa na wagonjwa wengine katika wodi moja.

Wakizungumza wakati wa kukabidhi rasmi jengo hilo lililojengwa na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera kupitia mradi wa Izigo, kinamama hao walisema tatizo la kuwachanganya wajawazito na waliojifungua na wagonjwa wengine, mbali na kuhatarisha maisha ya wanawake hao, pia ni hatari kwa usalama wa watoto wanaozaliwa maana wanaweza kuambukizwa magonjwa.

Mertha Clavery, alisema wamekuwa wakilazwa kati ya wawili hadi watatu katika kitanda kimoja kwa kuwachanganya na wagonjwa wengine kutokana na ufinyu wa wodi, na kuwa endapo jengo lililojengwa kwa ajili ya kinamama, litaanza kutumika matatizo hayo yatapungua au kuisha kabisa.

Naye Joyce Daud mkazi wa kijiji cha Kakindo, alisema uwapo wa jengo jipya utawaongezea faragha wajawazito wanaofika katika kituo hicho cha afya kujifungua na waliojifungua.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Izigo, Dk. Michael Butoyi, alisema ufinyu wa jengo hilo unawapa wakati mgumu na kuwa wakati mwingine walilazimika kuwashauri wagonjwa wengine kwenda Hospitali ya Kagondo inayomilikiwa na Kanisa Katoliki ili wapate huduma ya haraka.

Dk. Butoyi alisema mbali na ufinyu wa jengo, pia wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na gari la wagonjwa, hali inayosababisha baadhi ya wagonjwa wanaohitaji huduma zaidi kucheleweshewa huduma, kitendo kinachohatarisha usalama wa wagonjwa.

Naye Mkurugenzi wa Miradi wa World Vision makao makuu, Dk. Yosh Kasilima, akikabidhi jengo hilo, alisema kuwa mwaka 2018 walipokea ombi la kujengewa wodi ya kinamama kutoka kwa uongozi wa kituo hicho pamoja na ofisi ya mganga mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, na kuanza mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili hiyo, ambalo pia wananchi wamechangia nguvu zao.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima (kushoto), akipokea moja ya vitanda vya kawaida vya hospitali kutoka kwa Meneja wa Kanda ya Ziwa wa NMB, Abraham Augustino, kwenye hafla iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Buhare. Benki hiyo imetoa msaada wa Sh. milioni 50 ikijumuisha viti na meza 300 kwa ajili ya shule sita, mabati 222 kwa ajili ya shule moja, vitanda vya kujifungulia, mashuka na vitanda vya kawaida vya hospitali kwa ajili ya vituo vya afya vitatu vyote vya mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aagiza manispaa kumlipa mkandarasi shule

**Na Salome Kitomari**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Willium Ole Nasha, ameagiza Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, kumlipa mkandarasi anayekarabati Shule ya Sekondari Bukoba iliyoathiriwa na tetemeko la ardhi mwaka 2016.

Mkandarasi huyo amelipwa Sh. milioni 32 kati ya Sh. bilioni 1.4 zilizotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya ukarabati wa shue hiyo, jambo ambalo limefanya kazi hiyo kusuasua.

"Wizara imetoa fedha za kazi hii, lakini hadi sasa mkandarasi amelipwa Sh. milioni 32 kati ya Sh. milioni 200 alizotakiwa kulipwa, na kuagiza mkurugenzi dirisha likishafunguliwa hakikisha mkandarasi amelipwa fedha anazodai," alisema katika taarifa iliyopatikana jijini Dar es Salaam.

Waziri huyo alisema ukarabati wa shule hiyo unaoendelea umechelewa kukamilika kwani licha ya fedha hizo kupelekwa mapema, mkandarasi amechelewa kumaliza kazi kwa kadri ya muda uliopangwa.

Aidha, aliwataka watendaji wa manispaa hiyo kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo, kwa kuzingatia kubana matumizi kwa kuwa kuna uwezekano mkubwa wa fedha kubaki na kufanya shughuli nyingine za kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

"Nikifananisha fedha ambazo tumetumia kwenye maeneo mengine na miradi mingine mfano miradi ya afya ambayo wanatumia Sh. bilioni 1.5 kujenga majengo mapya makubwa saba, lakini hiyo Sh. bilioni 1.4 ambayo inakaribia na Sh. bilioni 1.5 ya afya tunakarabati majengo tu," alisema.

Aidha, alisema shule hiyo ina nafasi finyu ikilinganishwa na idadi kubwa ya wanafunzi 700 waliopo, huku akimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara kuwasiliana na Wakala wa Majengo ya Serikali (TBA) wenye eneo jirani na shule hiyo waangalie uwezekano wa kulimega kwa ajili ya shule hiyo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bukoba, Raymond Mutakyawa, alisema ukarabati huo ulikuwa ufanyike ndani ya siku 75 na ulipaswa kukamilika mwishoni mwa Julai, lakini ulisimama kutokana na kuchelewa kufunguka kwa mfumo wa malipo.

Shule hiyo inafanyiwa ukarabati baada ya kuharibiwa na tetemeko la ardhi mwaka 2016, baadhi ya majengo kuta zake kuanguka.



## HABARI ARUSHA

# Balozi wa Korea aasa matumizi mazuri ya rasilimali

**Na Allan Isack, ARUSHA**

BALOZI wa Korea nchini, Tae-ick Cho, amesema rasilimali zilizopo Tanzania, zikitumika vizuri zitawanufaisha wananchi wake kufikia malengo ya kiuchumi waliyojiwekea.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, katika hafla fupi ya kuzindua mradi wa kituo cha nishati ya umeme wa jua Tumaini Solar Plant, katika Kijiji cha Ngurdoto wilayani Arumeru, alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi na zikitumiwa vizuri zitawanufaisha wananchi kiuchumi.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi nzuri katika Bara la Afrika, ambayo imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi zikiwamo mbuga za wanyama, misitu, ardhi kubwa yenye rutuba na madini ya kila aina.

"Desemba mwaka jana nilipochaguliwa kuwa balozi wa Korea hapa Tanzania, nimekuwa nikijifunza utamaduni wa nchi hii, hususani kuzungumza lugha ya Kiswahili, kutokana na kuwa ni moja ya nchi zenye mvuto duniani, kwa sababu ya kuwa na sifa ya kuwa nchi yenye amani," alisema Ick Cho.

Alisema kuzinduliwa kwa mradi huo, kutawanufaisha wananchi wa eneo hilo kiuchumi, kwa kuwa watatumia nishati ya umeme katika shughuli za uzalishaji mazao, hususani kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Hata hivyo, alipongeza ushirikiano uliopo kati ya serikali ya Tanzania na Korea na alisema ushirikiano huo umelenga kuwasaidia wananchi katika sekta mbalimbali.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alisema mradi huo, umelenga kuzikomboa na kuziinua kaya maskini kujikwamua kimaisha na kiuchumi.

Alisema kijiji hicho, kilikuwa kinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma ya umeme, maji na shule ya sekondari, lakini kwa kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake, kwa kushirikiana na wananchi na wadau wa Kituo cha Utafiti cha Innovative Technology and Energy Center (iTEC), wamefanikiwa kutatua changamoto ya umeme kijijini hapo.

Alisema mradi huo wa umeme utawanufaisha wananchi zaidi ya 50, pia nishati hiyo itatumika kusukuma mtambo maalumu wa maji, ili wananchi waweze kulima kilimo chenye tija cha umwagiliaji.

Alitoa wito kwa wananchi wa eneo hilo, kulinda, kuutunza na kuuendeleza mradi huo, ili uweze kuleta matokeo chanya ya kimaendeleo kwenye kijiji hicho.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa mradi huo kutoka iTEC, Dk. Herb Rhee, alisema wametekeleza ujenzi wa miradi mitatu ya tumaini, urafiki na maisha. Alisema walitumia majina hayo, kwenye miradi hiyo, mitatu kwa kigezo cha kuwaunganisha watu, kuwa kitu kimoja kwa maslahi ya kimaendeleo.

Vile vile, alisema ujenzi wa mradi wa nishati ya umeme wa urafiki na tumaini, imeshakamilika na imeshakabidhiwa kwa wananchi, lakini mradi mwingine wa maji wa maisha upo katika hatua za mwisho kukamilika.

"Mradi wa kwanza wa tumaini tuliuzindua Januari katika Kijiji cha Mseserení, lakini kutokana na mahitaji ya nishati ya umeme wananchi walituomba kuongeza mradi mwingine wa umeme (urafiki), tulikubali maombi yao na utekelezaji wa mradi, ulifanyiwa kazi na sasa umekamilika na uzinduzi umefanyika Agosti 9, mwaka huu," alisema Rhee.

Alisema umeme huo wa nishati ya jua, una uwezo wa kuzalisha kilovoti 6.5 na utakuwa na nguvu ya kuwasha kwenye nyumba zaidi ya 50.

Alieleza kuwa hadi sasa jumla ya nyumba 46, zimeshaunganishiwa umeme na nyingine 40, zitaunganishiwa mwakani 2020 wakipata mradi mwingine.



Balozi wa Korea, Tae-ick Cho (watatu kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Jerry Muro, (wa pili kulia), wakikata utepe kuzindua kituo cha nishati ya umeme wa jua cha Tumaini Solar Plant, katika kijiji cha Ngurdoto na wa mwisho kushoto ni Meneja wa Mradi huo kutoka kituo cha utafiti cha iTEC Dk. Herb Rhee. **PICHA: ALLAN ISACK.**

## Madiwani wataka kampeni ya chanjo ya ini

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, limemwagiza Mganga Mkuu wa jiji hilo, Dk. Baraka Muondhe, kuendesha kampeni maalumu ya chanjo ya ugonjwa wa ini, ambao umekuwa tishio kwa binadamu na hauna dawa.

Agizo hilo limetolewa mwishoni mwa wiki na Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Karisti Lazaro kwa niaba ya madiwani wenzake, alipokuwa kwenye kikao cha baraza hilo kilichofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Arusha na kusisitiza kwamba kampeni hiyo ianze mara moja.

Aliiagiza Ofisi ya Mganga Mkuu wa Jiji hilo, kuhakikisha wananchi wanashirikishwa kikamilifu kupima afya zao na hataki kusikia mtu anapoteza maisha, kutokana na kutokuelimishwa ili wapime homa ya ini.

Akichangia hoja hiyo, Mbunge wa Viti Maalumu, Joyce Mukya, alisema ugonjwa huo ni hatari kuliko Ukimwi, hivyo Idara ya Afya isifanye mchezo na ugonjwa huo.

"Wenzetu wa Idara ya Afya wafanye hima kuhakikisha wanatilia mkazo suala hili la utoaji chanjo kwa wananchi wetu na kuwapa elimu ya ugonjwa huo, sababu ugonjwa huu unaua sana kuliko hata Ukimwi," alisema.

Alisema wananchi hawana elimu ya ugonjwa huo, ambao mpaka sasa hauna tiba, bali tiba yake ni chanjo hivyo wananchi wakipewa elimu watachukua tahadhari na kwenda kupima afya zao, kwenye vituo vya afya.

Akitoa ufafanuzi, Kaimu Mganga Mkuu wa Jiji la Arusha, Dk. Baraka Muondhe, alisema chanjo iliyokuwapo awali ilikuwa ikitolewa bure katika zahanati iliyopo Kata ya Daraja Mbili, lakini sasa chanjo hiyo imekwisha na inatolewa na zahanati binafsi.

Alisema kuwa wameshapeleka maombi ya kupatiwa chanjo hiyo, kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na itakapopatikana itatolewa kwa wananchi kuchangia gharama za chanjo hiyo ambayo itatolewa kwenye vituo vyote vya afya na zahanati za jiji hilo.

# Serikali yaagiza minada ya mifugo kuwekwa mizani

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imewaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kuweka mizani kwenye minada yote iliyopo chini ya halmashauri, ili wafugaji wapate tija na mifugo yao kwa kuuza kwa kilo, badala ya mapatano ya jumla bila kupima uzito wa mfugo husika.

Akitoa agizo hilo juzi katika Kijiji cha Mairowa, Kata ya Engaranaibo, wilayani Longido, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati alipotembelea eneo la mnada wa kata hiyo, alisema kukiwa na mizani, itasaidia wafugaji kunenepesha mifugo yao ili wapate maslahi mazuri.

"Nafahamu kukiwa na soko lenye mizani na kupima mifugo kwa kilo kabla ya kuuza kwa wafanyabiashara, itawageuza wafugaji wafuge kwa tija na kupata tija kwa sababu watakuwa wanauza kwa kufahamu kilo za mfugo wake na kupata bei stahili kama ilivyo kwa wauzaji wa biashara zingine kama korosho, mahindi na mengine," alisema.

Alisisitiza kusimamiwa kwa agizo hilo na Mkurugenzi wa Huduma za Masoko na Uzalishaji, Dk. Adam Nandonde na Mkurugenzi wa Bodi ya Nyama nchini, Imanuel Sechwale. Alisema wafugaji wanapata hasara kwenye mifugo yao kwa sababu ya ujanja unaotumiwa na wafanyabiashara ambao wananunua kwa mapatano ya kuangalia mfugo na wao kwenda kunufaika zaidi ya wafugaji kwa kuuza rejareja. Kukosa mizani, unakuta anauza nyama, lakini pembe, ngozi, kichwa, utumbo na miguu haipo kwenye kilo.

"Sasa hii hasara, kama Dar es Salaam unakuta bei ya pembe moja ni zaidi ya Sh. 15,000, lakini hivyo hapati mfugaji faida ya mfanyabiashara, lakini mfanyabiashara anauza utumbo, kichwa, ngozi, maini, kwato na vingine rejareja, hivyo vema sasa kila kitu kipimwe mnadani kwenye mizani wafugaji wapate stahiki yao," alisema na kuongeza:

"Iweje bidhaa zingine kama korosho zinauzwa kwa kilo kwa nini ng'ombe, mbuzi, kondoo wasiuzwe kwa kilo wakati mfanyabiashara ananufaika kwa kuuza kwa kilo kila kitu, sasa wafugaji nao wauze mifugo kwa kilo ili kuwasaidia kufuga kwa ushindani kwa kunenepesha mifugo yao iwe tija," alisema.

Alisema wafugaji wengi baada ya agizo hilo kutekelezwa watabadilika wenyewe na kuachana na ufugaji wa kuwa na mifugo mingi isiyo na tija, badala yake watafuga wachache wenye afya ili wapate kilo za kutosha.

Pia utaratibu ukiwekwa mzuri nchi nzima anaamini sekta hiyo itapata mabadiliko kwa haraka na viwanda vitapata malighafi bora na serikali kupata mapato mazuri, bila kusahau mfugaji.

Kuhusu uboreshaji wa majosho na dawa za mifugo, alisema serikali itahakikisha inakarabati majosho saba yanayotakiwa wilayani humo ambako kuna mifugo mingi na kupeleka dawa za kutosha.





## Aibuka mshindi wa Nanenane Kaskazini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI Maonyesho ya 26 ya Wakulima na Wafugaji katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini yakihitimishwa rasmi leo, baada ya serikali kuyaongezea siku nne zaidi, mkazi wa Kijiji cha Nganyeni katika Kata ya Mwika Kaskazini, Wilaya ya Moshi, Elinaja Mlay, ametwaa nafasi ya pili ya mkulima bora wa mwaka 2019.

Mlay ambaye ni mkulima maarufu wa kahawa, amekuwa akiendesha shughuli zake za kilimo katika Wilaya ya Moshi, kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Pia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imeng'ara katika maonyesho hayo ya Nane nane, kwa kuwa mshindi wa kwanza wa banda bora la mifugo, kati ya mabanda yote yaliyoshiriki maonyesho hayo kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara.

Agosti 8 mwaka huu, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, akiwa katika maonyesho hayo ya mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara kwenye viwanja vya Themi, alisema serikali imeamua kuongeza siku nne zaidi za kufanyika kwa maonyesho hayo ya wakulima na wafugaji ili kutoa fursa zaidi kwa wananchi kupata fursa ya kuona kinachofanywa na wakulima na wafugaji.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum baada ya kutwaa tuzo hiyo, Mlay alisema ushindi huo ni wa wakulima wote wa Moshi wanaozingatia masharti ya kilimo bora na kwamba kama serikali itautekeleza kwa vitendo mkakati wa kusajiliwa wakulima utasaidia kupata taarifa zao za msingi na kuweza kuhudumiwa.

"Nafahamu kuwa serikali inao uwezo wa kuwahudumia wakulima kwa kuweka miundombinu imara, kutengeneza sera, sheria, kanuni na kusimamia utekelezaji wa sera za kilimo kufuatana na mipango yake.

Zaidi aliongeza: "Ukweli kwa mazingira ya kilimo huria, hivi sasa imekuwa ni tatizo sana kuwa na taarifa za kutosha kwa serikali za kuiwezesha kupanga mipango ya uhakika ya kilimo, kiuchumi na huduma kwa wakulima na watu wake, hata hivyo kwa asilimia kubwa ushindi wangu unatokana na juhudi binafsi."

Aidha, Mlay amezishauri Halmashauri za Wilaya katika mikoa hiyo kuwajengea wakulima uwezo zaidi wa kulima, kusindika na kuuza bidhaa zilizoongezewa thamani katika masoko ya wakulima ambayo wanashiriki kupanga bei badala ya kupangiwa bei.

Alisisitiza kuwa mkulima ambaye yuko kwenye kilimo mseto, atakuwa anauza bidhaa mbalimbali kutokana na shughuli za kilimo, ufugaji, uvuvi na mazao ya misitu na kipato chake kitakuwa kikubwa kama atauza bidhaa zilizoongezewa thamani kwa bei ambayo mkulima anashiriki kupanga kwa mwaka mzima.

# Hifadhi ya Mkomazi yaanzisha tuzo maalum

**Na Godfrey Mushi,** SAME

HIFADHI ya Taifa ya Mkomazi, imeanzisha tuzo maalum ya jamii na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kutambua, kuthamini na kuchochea masuala ya ulinzi wa ikolojia kuzunguka maeneo ya hifadhi hiyo.

Mpango huo wa Mkomazi kuanza kutoa tuzo hiyo kuanzia mwaka huu, uliwekwa wazi mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule.

"Nimefurahishwa sana na namna Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ilivyojiwekea mkakati maalum wa kulinda ikolojia katika maeneo yanayozunguka hifadhi hiyo, hasa baada ya mimi kuitwa kukabidhi tuzo hiyo kwa washindi watano wa vikundi pamoja na shule tano zilizofanya vizuri. Wameanza vyema kwa kutoa fedha kati ya Sh. 200,000 hadi Sh. 700, 000.

"Wamenieleza wameanzisha tuzo hiyo kwa jamii na taasisi mbalimbali zinazozunguka hifadhi hiyo ili kuisukuma jamii kujali na kutunza ikolojia ya hifadhi kuanzia mwaka 2019. Ni vizuri na wengine wakaiga mfano huo."

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi, Abel Mtui, alisema tuzo hiyo inalenga kuongeza mwamko wa jamii kulinda rasilimali za nchi zilizopo katika hifadhi hiyo.

Kamishna huyo ameahidi tuzo hiyo itakuwa endelevu kila mwaka, huku akiiasa jamii kuona umuhimu wa kuitunza na kuilinda Hifadhi ya Mkomazi kama rasilimali ya kujivunia kwa Wilaya ya Same.

Alisema mpango hifadhi hiyo wa kuwatumia faru kama kivutio pekee cha utalii kitakachoitambulisha tofauti na hifadhi nyingine nchini, utaifanya Mkomazi kuwa hifadhi pekee Tanzania yenye kivutio hicho.

Mkomazi hutumika kama kituo kwa ndege ambao husafiri kati ya Bara Ulaya na Afrika. Ni hifadhi inayowavutia wageni wa kimataifa wanaopenda kuangalia aina mbalimbali za ndege.

Ndege hao wanaohama hutumia maeneo ya hifadhi kama vituo vyao vya kupumzikia wakiwa wanaelekea Kusini mwa Afrika au kipindi wanapokuwa wanarudi makwao katika Bara la Ulaya.

Lakini pia, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi imesheheni wanyama kama swala, twiga, cholawa, simba, faru, tembo, pundamilia na mbwa mwitu ambao hutembea kwa makundi na kuwa kivutio kikubwa kwa watalii.

Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ilianzishwa mwaka 2007 na inapakana na Pori la Akiba la Wanyamapori la Umba lililopo mkoa wa Tanga.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella (wa pili kushoto), akisalimiana na Mbunge wa Jimbo la Muheza, Balozi Adadi Rajabu, jana wakati akitoka katika mkutano wa hadhara katika kata ya Kwabada, wa kwanza kushoto mwenye baibui Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Utajiri wa madini Mwanga watajwa changamoto kubwa

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

UTAJIRI wa madini ya shaba na jasi (Gypsum) yanayopatikana kwa wingi katika Wilaya ya Mwanga, bado uwekezaji wake haujaweza kuwa na tija, zaidi ya kuchimbwa kwa kiwango cha chini na wachimbaji wadogo.

Kwa mujibu wa taarifa zinazohusu fursa ya uwekezaji kwenye madini, iliyowekwa katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, madini mengi hadi sasa hayajachimbwa ama yanachimwa kwa kiwango kidogo.

Zaidi taarifa hiyo imeeleza, madini ambayo yanachimbwa kwa wingi na yanaipatia halmashauri hiyo mapato kwa kiasi kikubwa ni madini ya ujenzi yanayotokana na uchimbaji wa mchanga. Madini ya shaba yanapatikana kwa wingi katika maeneo ya Vuchama-Ndambwe katika Kata ya Shighatini na madini ya jasi yanayapatikana katika eneo la Njia Panda, Kata ya Kirya.

Uzalishaji wa madini ya gypsum nchini ni tani 354,000 na mahitaji ya soko ni tani 30,000 kwa mwezi katika viwanda vya saruji nchini. Maeneo mengine yenye madini hayo ya gypsum ni Lindi, Itigi na Simiyu. Jasi inayopatikana Tanzania inatajwa kuwa ni ya ubora wa hali ya juu na nyingine kufikia kiwango cha ubora wa asilimia 98.

Aidha, madini ambayo yanachimbwa kwa wingi na yanayotegemewa kwa mapato ya ndani na halmashauri hiyo ni chokaa yanayochimbwa eneo la Kisangara katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mwanga.

Mengine ni udongo mweupe unaopatikana katika eneo la Lambo, Kata ya Shighatini na madini ya kokoto yanayopatikana kwa wingi 'Kwanyange' huko katika Kata ya Kivisini.

Kutokana na utajiri huo wa madini uliopo pia maeneo mbalimbali nchini, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, amekuwa akisisitiza kuwa ipo haja ya kuwahimiza wawekezaji au wachimbaji wenye leseni kuwekeza katika mitambo ya kuchenjulia madini ili kuyaongezea thamani, kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

NIPASHE JUMATATU AGOSTI 12, 2019

Nipashe

Spotika



KLABU EPL ZILIVYOTUMIA FEDHA KWENYE USAJILI UK.20



# HAT-TRICK...

Mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling, akikamilisha hat-trick yake wakati wakishinda 5-0 kwenye mechi yao ya ufunguzi wa Ligi Kuu England dhidi ya West Ham iliyopigwa Uwanja wa London. Kushoto anayejaribu kumzuia bila mafanikio ni Declan Rice. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

David Luiz amekuwa mchezaji wa 10, kuzichezea klabu zote mbili Arsenal na Chelsea tangu Ligi Kuu England kuanza kuitwa Premier League. Mbrazil huyo amefuata watangulizi wake Emmanuel Petit, Ashley Cole, Nicolas Anelka, William Gallas, Petr Cech, Yossi Benayoun, Cesc Fabregas, Lassana Diarra na Olivier Giroud. Arsenal imemnasa Luiz kwa pauni milioni nane majira haya ya joto.

# MSIMU MPYA EPL KUNA JIPYA GANI?



Aguero

Guardiola

**LONDON, England**

PAZIA la Ligi Kuu ya England msimu wa 2019/2020 limefunguliwa rasmi Ijumaa.

Msimu uliopita 2018/2019, ulikuwa ni moja ya misimu bora na wenye ushindani wa hali ya juu. Je, mambo yatakuwaje kwenye msimu huu mpya.

Mshindi wa Ligi Kuu msimu uliopita Manchester City na mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Liverpool, walimaliza kwa kupishana kwa pointi moja tu katika ligi.

Liverpool ilimaliza msimu ikiwa na pointi 97, ambazo ni nyingi kuwahi kukusanywa na mshindi wa pili. Jurgen Klopp atataka kuhakikisha anampiku Pep Guardiola safari hii.

Msimu wa 2019/19 Liverpool na Manchester City walibadilishana nafasi ya kileleni zaidi ya mara kumi kwenye mbio za kuwania ubingwa wa EPL na kuonyesha uhasama wa aina yake huku wakicheza kandanda ya kuvutia na kasi ya kusisimua.

Uhasama huo bila shaka utaendelea tena msimu huu na ushahidi ni mchezo wa Ngao ya Jamii ambao ulichezwa kama fainali kwenye Uwanja wa Wembley, kila upande ukitaka kushinda mechi hiyo. Kwa Liverpool na City, unaweza kusema huu si msimu mpya kwao bali ni mwendelezo wa msimu uliopita.

Liverpool walipoteza mchezo huo kwa matuta, baada ya kukosa mkwaju mmoja wa penalti, lakini tulipata nafasi ya kuona kionjo cha jinsi msimu utakavyokwenda kwa timu hizi mbili ambazo ni kama 'wababe wapya' katika Ligi Kuu ya England ambayo ilikuwa ikitawaliwa na Manchester United, Chelsea na Arsenal katika robo karne iliyopita.

Lakini sasa mtaani kuna 'vichwa' vipya, na katika takriban miaka kumi iliyopita, tunashuhudia kilele cha EPL kikianza kutawaliwa na waliokuwa 'wanyonge'.

Man City, Liverpool na Tottenham wameingia kwenye picha na hakuna dalili zozote zinazoonyesha kuwa wataondoka hivi karibuni.

EPL ambayo kwa miaka mingi ikifahamika kuwa na "Top 4" sasa imebadilika na kufika "Top 6" kwa sababu ya ushindani ambao umeongezeka katika miaka ya hivi karibuni, hasa kutokana na kuingia kwa wababe wapya.

Nafasi tatu za juu, kama msimu uliopita, wengi wanatarajia kugombewa na Tottenham, Man City na Liverpool. Nafasi tatu zilizosalia za top 6 zinatazamiwa kugombewa na Arsenal, Chelsea na Manchester United.

Lakini kama tulivyoshuhudia msimu uliopita, nafasi hizo 'hazijathibitishwa' kwa sababu kuna timu kama Everton na Wolverhampton ambazo kwa jinsi zilivyocheza zinaweza kutikisa na kuingia ndani sita bora.

Je, Solskjaer ataweza kuiongoza Man United mpaka kuchukua ubingwa msimu huu? Ama mashabiki wataendelea kusubiri?

Licha ya kuwa msimu huu fedha nyingi hazijatumika kwenye usajili ukilinganisha na misimu miwili iliyopita, utakuwa msimu mgumu hasa kwa makocha wapya katika timu za juu- kama vile Frank Lampard, Ole Gunnar Solskjaer na hata Unai Emery ambaye unaweza kusema ndio kwanza anaunda kikosi chake baada ya miaka zaidi ya 20 ya Arsene Wenger.

Kwa upande wa chini wa msimamo, katika miaka kumi iliyopita, timu mbili kati ya tatu zinazopanda daraja hufanikiwa kusalia kwenye ligi.

Ni mara tatu tu katika historia ya Ligi Kuu ya England ambapo timu zote tatu zilizopanda daraja zilifanikiwa kuepuka kushuka daraja katika msimu ambao zilipanda.

Msimu huu teknolojia ya maamuzi kwa njia ya video, VAR, itatumika kwa mara ya kwanza na hivyo kuongeza chachu katika ligi hii maarufu na yenye ushindani duniani.

Na sheria nyingine kadhaa pia zitatumika, ikiwamo ya kudhibiti makocha 'wakorofi' kwa kuonyeshwa kadi za njano kama onyo na pia sheria ya wachezaji wanaobadilishwa hutakiwa kutoka uwanjani haraka kuepuka kupoteza muda.

Msimu ni mpya, na EPL miaka yote hushangaza wengi kwa kuleta kitu kipya, lakini kwenye karatasi unaweza kubashiri nani ana nafasi kubwa ya kuwa bingwa, na nani ana nafasi kubwa ya kushuka daraja.

Hata hivyo, burudani itakuwa katika timu zile ambazo zinataka kwa udi na uvumba kurejesha 'heshima' zake.

**JE, WAJUA?**



Nicolas Pepe (kwa sasa Arsenal) ni mmoja kati ya wachezaji wawili waliofunga mabao 20 na zaidi na kutoa pasi za mwisho 10 na zaidi, katika ligi bora tano za Ulaya kwenye msimu wa 2018/19 (akifunga mabao 22 na pasi za mwisho 11), nyuma ya Lionel Messi.

# 10-BORA

## YA USAJILI GHALI ZAIDI ULAYA

**LONDON, England**

USAJILI wa kipindi hiki cha majira ya joto umeonekana kwa timu kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya barani Ulaya na hadi sasa wakati kwa dirisha la England limefungwa huku kwingine usajili ukiendelea. Hapa tunaangalia 10-bora ya usajili ghali zaidi Ulaya hadi kufikia sasa...

**Hazard - Chelsea kwenda Madrid - Pauni Mil. 130**

Iilikuwa ni habari ambayo mashabiki wengi wa Chelsea walikuwa wakiihofia, lakini hatimaye Eden Hazard akaamua kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Real Madrid mwanzoni mwa Julai, akihamia katika klabu ambayo aliota kuichezea tangu utoto wake. Alinunuliwa na Real Madrid kwa pauni milioni 130.

Hazard atakumbukwa kama mmoja wa wachezaji wakubwa zaidi wa Chelsea akiwa ameichezea mechi 352, akifunga mabao 110, akishinda mara mbili taji la Ligi Kuu ya England, mataji mawili ya Europa, na mara moja Kombe la FA na lile la Ligi. Na sasa akili yake ni kuisaidia Real Madrid na yeye kufikia kwenye kiwango cha juu zaidi.

**Felix - Benfica kwenda Atletico - Pauni Mil. 113**

Atletico Madrid ilishinda mbio za kuwania saini ya Joao Felix kutoka Benfica, lakini walilazimika kulipa kiasi cha pauni milioni 113 ili kumpata mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 na sasa wanasubiri kuona makali yake kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu.

Felix atakuwa na jukumu la kubeba mikoba ya Antoine Griezmann kwenye kufunga mabao baada ya msimu uliopita kufunga mabao 20 katika mechi 43 alizoichezea Benfica.

**Griezmann - Atletico kwenda Barcelona - Pauni Mil 108**

Antoine Griezmann kipindi cha majira ya joto kilichopita aliwashtua wengi kwa kuamua kukataa ofa ya kujiunga na Barcelona na kuamua kubakia pale Atletico Madrid, lakini safari hii ameamua kuondoka. Ada ya pauni milioni 108 ambayo imezusha utata kwa Atletico kutaka fedha zaidi, imemfanya mchezaji huyo kuondoka kwenye klabu hiyo yenye makao yake makuu mji mkuu wa Hispania.

Hata hivyo, Griezmann kwa sasa ameshatua zake pale Nou Camp na sasa atacheza kwa pamoja na Lionel Messi na Luis Suarez, na wanatarajia kutengeneza safu moja kali zaidi ya ushambuliaji barani Ulaya. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, alifunga mabao 133 katika misimu mitano aliyokaa Atletico na sasa atahamishia nguvu hizo pale Barcelona.

**Maguire - Leicester kwenda Man United - Pauni Mil. 80**

Manchester United ilikuwa na uhitaji mkubwa wa beki wa kati kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake, na kipindi hiki cha majira ya joto wamefanikiwa kutatua tatizo hilo kwa kumsajili Harry Maguire ambaye ameweka rekodi ya kuwa beki ghali zaidi duniani kwa sasa.

United walijaribu kutaka kumsajili Maguire baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018, lakini baada ya miezi 12 wameweza kuipata saini ya beki huyo wa kimataifa wa England na sasa anatarajia kumaliza tatizo la beki pale Old Trafford.

**Lukaku - Man United kwenda Inter Milan - Pauni Mil. 73**

Safari ya Lukaku kuondoka Man United ilikuwa ni suala la muda tu kwani yeye mwenyewe alishabainisha wazi anataka kutondoka. Na hakuhusishwa kwenye mechi za maandalizi ya msimu mpya nchini Australia na mashariki ya mbali. Wakati Juventus waliposhindwa kumsajili katika uhamisho ambao ungemhusisha Paulo Dybala, Inter wakatia mguu na kumsajili mshambuliaji huyo.

**Pepe - Lille kwenda Arsenal - Pauni Mil. 72**

Kulikuwa na uvumi kwamba, Arsenal walikuwa na bajeti ndogo ya usajili ikiwa ni pauni milioni 45 pekee ambazo zilitengwa kwa kipindi hiki cha majira ya joto, lakini wakaweza kufanikisha usajili wa pauni milioni 72 kwa kumsajili mshambuliaji wa Lille, Nicolas Pepe mwanzoni mwa Agosti.

Mshambuliaji huyo alikuwa na wakati mzuri akicheza pale Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, msimu uliopita akifunga mabao 23 na pasi za mwisho 12 katika mechi 41, na sasa anatarajia kuungana na Alexandre Lacazette na Pierre-Emerick Aubameyang kwenye fowadi ya Arsenal.

**De Ligt - Ajax kwenda Juventus - Pauni Mil. 67.8**

Juventus ilitumia fedha nyingi kumchukua Matthijs de Ligt ili atue nchini Italia kipindi hiki cha majira ya joto na mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia mwenye umri wa miaka 19, ameondoka kwenye klabu yake ya utotoni ya Ajax ambayo alifika nayo nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

De Ligt, alikuwa nahodha mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya Klabu ya Ajax, alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua Manchester United na Barcelona, lakini Juventus ikashinda kwenye mbio za kumwania na akasajiliwa.

**Hernandez - Atletico kwenda Bayern- Pauni Mil. 68**

Bayern Munich ilivunja rekodi yao ya usajili kwa kumchukua mshindi wa Kombe la Dunia, Lucas Hernandez katika klabu hiyo akitokea Atletico Madrid, na 'dogo' huyo mwenye umri wa miaka 23 sasa atakuwa na wakati wa kujiimarisha zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Hata hivyo, Hernandez wakati akifanyiwa vipimo vya afya alionekana ameumia kwenye goti lake na kutakiwa kufanyiwa operesheni, lakini miamba hao wa Ujerumani waliamua kumsajili hivyo hivyo na anatarajia atakuwa fiti kabla ya kuanza kwa msimu mpya.

**De Jong - Ajax kwenda Barcelona - Pauni Mil. 65**

Matthijs de Ligt si mchezaji kijana pekee aliyeondoka Ajax kipindi hiki cha majira ya joto, kwani kiungo Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 21 naye amejiunga na Barcelona kwa pauni milioni 65.

Klabu ya Ajax imepata faida kubwa kwa kumuuza De Jong ambaye walimnunua kutoka Willem II kwa pauni 260,000 kipindi cha majira ya joto mwaka 2015, na sasa Mholanzi huyo ana jukumu kubwa na kuimarisha kiungo cha Barcelona

**Ndombele - Lyon kwenda Tottenham - Pau Mil. 63**

Wakati Lyon walilipa pauni milioni saba pekee kumtwaa kiungo huyo wa kati miezi 12 iliyopita, Tottenham wametumia fedha nyingi kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ambaye anaonekana atakuwa nguzo ya kocha Mauricio Pochettino msimu huu.

Na sasa Ndombele anatarajiwa kuibeba Spurs kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu ya England ulioanza Ijumaa.




Hazard



Antoine-griezmann

## Nukuu

"Katika maisha, mara zote nimekuwa nikipenda kufanya changamoto kadhaa kila wakati. Siogopi hata kujaribu vitu. Nadhani si wachezaji wengi sana wangefanya aina hii ya uhamisho, labda wangeogopa, au kitu kama hicho. Ninajaribu tu kufanya vitu vikubwa katika maisha yangu, hivyo ninasema mzunguko wangu Chelsea umemalizika na nina furaha kuanza ukurasa mpya wa maisha yangu hapa. Arsenal ni klabu kubwa - na si tu kwa England, bali kila mtu duniani anajua ni kwa namna gani ilivyo kubwa," **David Luiz**



"Bahati nzuri kwake, siwezi kusema chochote kuhusu hilo kwa sababu kila mara kutakuwa na wakati ambapo itabadilika, hilo ndilo soko. Yeye hana ushawishi wowote kwa hilo, lakini ninamtakia kila la heri. Dau kubwa linakuja na presha, lakini haibadili sana kwa sababu mara zote unakuwa na presha katika klabu kubwa kama Man United. Lakini ninamtakia heri," **Beki wa Liverpool, Virgil van Dijk akimhasa Harry Maguire wa United baada ya kuvunja rekodi yake ya kununuliwa kwa dau kubwa.**



"Kama ilivyo leo (Jumanne iliyopita), hakuna suala la Neymar, kama rais alivyosema, na kuna utata. Sisi ni watendaji tu, tunajua hana furaha Paris na ni hali ambayo inahitaji kutatuliwa Paris, hatujazungumza nao. Kuna heshima kubwa kati ya klabu hizi na kama kuna suala la Neymar siku moja, tutazungumza. Leo (Jumanne iliyopita), kwa wakati huu, limewekwa kando," **Makamu Rais wa Barcelona, Jordi Cardoner.**





Beki wa Yanga, Paul Godfrey akipiga hesabu ya kuwazuia wachezaji watatu wa Township Rollers kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Taifa Jumamosi.

# SABABU 5 SARE SIMBA, YANGA LIGI YA MABINGWA

**Na Adam Fungamwango**

SARE tatu za mechi za kimataifa kwa timu za Tanzania zilipatikana siku ya Jumamosi kwenye viwanja na nchi mbalimbali.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Simba wakiwa nchini Msumbiji kwenye mji wa Beira, walitoka suluhu ya bila kufungana na UD Songo katika pambano kali la aina yake la Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Yanga ikiwa mbele ya mashabiki wake, ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Township Rollers ya nchini Botswana kwenye mechi nyingine ya Ligi ya Mabingwa.

Timu mpya kabisa iliyopanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu uliopita, KMC, ilifanya maajabu baada ya kutoka sare dhidi ya AS Kigali, si tu ikicheza kwa mara ya kwanza michuano ya kimataifa, lakini pia ikicheza ugenini.

Kwa matokeo hayo ni kwamba timu hizo tatu zinahitaji matokeo chanya kwenye mechi za marudiano zitakazofanyika wiki mbili zijazo.

Yanga ndiyo itakuwa na kazi kubwa kwa sababu italazimika kwenda kupambana ugenini nchini Botswana, wakati Simba itakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Taifa, ambao mara nyingi si salama kwa timu ngeni zinapofika hapo.

KMC pia ina nafasi kubwa ya kusonga mbele kwani suluhu iliyoipata ugenini imeipa moyo na kiburi cha kupambana ikiwa kwenye ardhi ya nyumbani.

"Tumefanya kitu kizuri kutoruhusu bao. Pamoja na juhudi kubwa za wapinzani, lakini wachezaji wangu walikaa imara, tutajiandaa kwa ajili ya mchezo wa marudiano. Mchezo wetu wa marudiano tuna nafasi ya kufanya vizuri, tunaomba mashabiki wetu watupe sapoti," alisema Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems.

"Kwa sasa hesabu ni kwamba tutakuwa na kikosi imara ambacho kitapata matokeo kwenye mchezo wetu wa marudiano, mashabiki waendelee kutupa sapoti katika hili, nami nitafanyia kazi makosa yote," Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera naye anaongeza maneno hayo.

Kwa jicho la mchambuzi wa makala haya, hizi ndizo sababu zilizofanya timu hizo kupata sare kwenye mechi hizo za mkondo wa kwanza.

**1. Simba, Yanga hazina muunganiko**

Bado timu za Simba na Yanga hazina muunganiko kutokana na kuwa na baadhi ya wachezaji wageni.

Yanga ndiyo iliyoongoza kwa kuchezesha wachezaji wengi wageni, tofauti na wale waliokuwa kwenye kikosi hicho msimu uliopita. Ni wachezaji wawili wa zamani tu ambao walianza mechi hiyo ambao ni Paul Godfrey na Papy Tshishimbi pekee, huku Mrisho Ngassa akiingia kipindi cha pili.

Hata Kocha Mkuu wa Yanga, Zahera amekiri hilo na kusema kuwa wachezaji wake bado wana tatizo la kushindwa kuelewana wakiwa ndani ya uwanja jambo ambalo linaleta ugumu kupata matokeo uwanjani.

Simba nayo iliathiriwa na hali hiyo, ingawa si sana kwa sababu Aussems alijitahidi sana kutopanga wachezaji wengi wageni na badala yake akaziba mapengo ya wachezaji ambao wameondoka.

Wachezaji wapya ambao Simba iliwapanga kwenye mechi hiyo ni Benno Kakolanya na hii ni kwa sababu Aishi Manula ni majeruhi, wengine wakiwa na Gadiel Michael, Sharaf Eldin Shiboub, Francis Kahata, na baadaye aliingia Deo Kanda.

**2. Michuano kuanza kabla ya Ligi Kuu**

Michuano ya Ligi ya Mabingwa pamoja na Shirikisho barani Afrika kuanza kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara haijaanza nayo imekuwa ni majanga, kwani imesababisha timu za Simba na Yanga kutokuwa kwenye muunganiko na wachezaji kuwa bado hawajaelewana.

Kocha wa Simba alishawahi kulalamika kuwa walishtukizwa na ratiba hiyo kwani walitegemea kuwa wangeanzia kwenye raundi ya kwanza na si ya awali.

Hii ina maana kuwa bado alikuwa hawajajiandaa na michuano hiyo, lakini kwa sababu imekuja kwa kushtukiza, akabadili aina ya mazoezi ili mradi kuendana na matakwa ya mechi za awali.

Kwa jinsi timu hizo zilivyo, kama zingeanza na mechi za Ligi Kuu angalau tatu ama nne, halafu ziende kwenye mechi za kimataifa, tungeweza kushuhudia timu zote mbili zikitinga hatua inayofuata kirahisi.

**3. Zahera kuchelewa kurudi**

Yanga pamoja na kuonekana ina baadhi ya wachezaji wapya wenye uwezo mkubwa, lakini bado inaathiriwa na vitu vingi vya kiufundi na hii inasababishwa na Kocha Mkuu, Zahera kuchelewa kurejea kutoka kwenye mapumziko.

Zahera alirejea wiki moja tu kabla ya Yanga kuanza michuano hiyo, na ingawa si viongozi wa Yanga wala mashabiki wao waliokemea jambo hilo, lakini hili limeigharimu sana timu hiyo kwenye mechi hiyo. Na hata kama itatolewa kwenye michuano hiyo, Zahera ni lazima abebe lawama hiyo na wala si wachezaji wake.

**4. Simba kuanza kuheshimu wapinzani**

Simba imepata sare kwa mara ya kwanza ugenini na hii ni tofauti na msimu uliopita. Kwenye Ligi ya Mabingwa msimu uliopita ilipata ushindi kwenye mechi moja tu dhidi ya Mbabane Swallow ya Eswatini zamani ikiitwa Swaziland, huku ikipokea vichapo kwenye mechi zingine zote za ugenini.

Kocha wa Simba anaonekana safari hii amebadilisha mbinu na kucheza mfumo wa kujilinda zaidi timu inapokuwa ugenini kuliko kushambulia zaidi ambapo huwapa mwanya wapinzani.


Kwenye mechi dhidi ya UD Songo, Simba ilionekana kutafuta zaidi sare kwani ilishambulia mara chache na kujilinda zaidi.

**5. KMC ilicheza sehemu ilipozoea**

Mwezi mmoja tu uliopita, timu ya KMC ilikuwa nchini Rwanda kwenye michuano ya Kombe la Kagame. Michuano hiyo iliyoanza Julai 6 hadi 19, si tu kwamba iliifanya KMC inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni kupata angalau uzoefu kidogo, lakini pia kuizoea nchi ya Rwanda, hasa Kigali kiasi kwamba hata ilipopangiwa dhidi ya AS Kigali haikuhofu sana kwa sababu ni sehemu ambayo wanaifahamu.

Ndiyo maana hata mechi yenyewe KMC ilicheza soka safi bila hofu kwa sababu tayari walikuwa wameshaizoea nchi hiyo kwa kila kitu kiasi cha kuwapa tabu wapinzani wao.

**NAJUA WAJUA**



MOHAMED Salah ameifungia Liverpool katika kila mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu England kwenye misimu mitatu aliyoicheza (msimu wa 2017-18, 2018-19 na 2019-20).

SOKA

# 6-BORA
## EPL ILIYOLAMBA DUME USAJILI 2019/20


Unai Emery

**LONDON, England**

PAZIA la dirisha la usajili kwa Klabu za Ligi Kuu ya England lilifungwa rasmi Alhamisi ya Agosti 8, mwaka huu.

Ulikuwa ni wakati ambao klabu sita za Ligi Kuu ya England kupigana na kuhakikisha zinakamilisha usajili wao dakika za mwisho kabisa.

Hapa tunaangalia kwa ukaribu klabu gani katika sita bora iliyofanya usajili bora zaidi.

**6. Liverpool**

Mabingwa hawa wa Ligi ya mabingwa Ulaya, hawakuwa na mambo mengi zaidi kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto. Walimsajili golikipa Adrian kuchukua nafasi ya Simon Mignolet aliyeondoka, kwani makinda Sepp van den Berg na Harvey Elliott walikuwa ndio pekee walioongezwa. Bado wao wana imani kubwa na wachezaji wao wa msimu uliopita. Je, wataweza kushindana na Manchester City kwenye mbio za Ligi Kuu ya England msimu huu? Ni suala la kusubiri kuona...

**5. Manchester United**

Wakati wakiwa wamemwachia Romelu Lukaku kwenda Inter Milan kwa pauni milioni 73 pengine ulikuwa ni wakati mwafaka kwa wao kutafuta mchezaji wa kurithi mikoba yake. Hivyo kushindwa kumwongeza mshambuliaji mwingine, kunaiweka fowadi ya United kwenye wakati mgumu kidogo. Harry Maguire alisajiliwa na kufanywa kuwa beki ghali zaidi duniani ambaye walimsajili kwa pauni milioni 80 kutoka Leicester City, pia wakiwachukua Aaron Wan-Bissaka na Daniel James.

**4. Chelsea**

Chelsea hawakuingia kwenye usajili wakiwa wanatumikia adhabu ya kutofanya usajili kwa msimu wa 2019-20, lakini waliweza kumpata Mateo Kovacic aliyesaini mkataba wa kudumu na Christian Pulisic ambaye angalau atapoza machungu ya kuondoka kwa Eden Hazard aliyetimikia Real Madrid. Chelsea wamempeleka Danny Drinkwater kule Burnley kwa mkopo hadi Januari 6 na wamemruhusu David Luiz kuondoka kwenda Arsenal kwa pauni milioni nane siku ya mwisho ya usajili.

**3. Manchester City**

Pep Guardiola hatimaye alimpata mrithi wa Fernandinho, Rodri, ambaye alitua hapo kutokea Atletico Madrid. Mpango wa Danilo kumpeleka Juventus umewafanya wampate Joao Cancelo. Scott Carson na Pedro Porro walitua hapo katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili na wameweza kumbakiza Leroy Sane ambaye sasa atafanyiwa upasuaji wa goti lake la kulia baada ya kuumia kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii Jumapili iliyopita dhidi ya Liverpool. Ingawa Bayern Munich ambao wanamwania kwa udi na uvumbi wana nafasi hadi Septemba 2 kuweza kumsajili, kwani siku hiyo ndio dirisha lao la usajili linafungwa nchini Ujerumani.

**2. Tottenham**

Wachezaji wawili wameongeza 'utamu' wa Tottenham Hotspur kwenye Ligi Kuu, huku wakimchukua Tanguy Ndombele kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo pamoja na Giovani Lo Celso ambaye ametua kwa mkopo na kuna kipengele cha kumnunua moja kwa moja. Siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili wakampata Ryan Sessegnon kwa ada ya pauni milioni 25.

**1. Arsenal**

Washika Bunduki hawa kutoka Kaskazini mwa Jiji la London walimsajili Nicolas Pepe aliyejiunga kutoka Lille kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 72, huku wakimpata Dani Ceballos waliyemchukua kwa mkopo kutoka Real Madrid. Gabriel Martinelli ameongeza nguvu kwenye safu ya ushambuliaji, huku kwenye ulinzi Kieran Tierney ametua kuongea nguvu akitokea Celtic kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 25 pamoja na David Luiz kutoka Chelsea. Arsenal iliamua kumuuza Alex Iwobi aliyekwenda Everton kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 34 na pia waliweza kupata pauni milioni 4.6 baada ya kumuuza nahodha wao, Laurent Koscielny ambaye aliweka wazi kuwa anataka kuondoka klabuni hapo.

**NDANI YA 18**



Raheem Sterling amekuwa mchezaji wa nane kufunga hat-trick katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu England, na wa kwanza tangu Didier Drogba alipofanya hivyo msimu wa 2010-11.




USAJILI wa kipindi hiki cha majira ya joto umeonekana kwa timu kutumia kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya barani Ulaya na hadi sasa wakati kwa dirisha la England limefungwa huku kwingine usajili...

Uk. 16-17

# KLABU EPL ZILIVYOTUMIA FEDHA KWENYE USAJILI




Solskjaer

**LONDON, England**

NI kiasi gani kimetumika na Klabu za Ligi Kuu ya England wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, makala haya yanakuchambulia kwa kina kiasi kilichotumika na rekodi iliyowekwa kwa wachezaji waliosajiliwa.

Klabu za Ligi Kuu kwa pamoja zimetumia kiasi cha pauni bilioni 1.4 kwa usajili wa wachezaji 114 kipindi hiki cha majira ya joto, lakini kila timu imetumia kiasi gani?

Harry Maguire ndiye alikuwa mchezaji ghali zaidi kwa dirisha la usajili na pia amekua beki ghali zaidi duniani baada ya Manchester United kulipa kiasi cha pauni milioni 80 ili kupata huduma yake.

Arsenal walitumia kiasi cha pauni milioni 72 kumsajili mshambuliaji wa Lille, Nicolas Pepe, huku usajili mwingine wa bei ghali ukiwa ni wa Tanguay Ndombele (pauni milioni 63 kwenda Tottenham) na Manchester City wakimsajili Rodri (pauni milioni 62.5) na Joao Cancelo (pauni milioni 60).

**KLABU ZILIVYOTUMIA**

**Manchester United**

Inaongoza kwenye orodha ya ya klabu iliyotumia kiasi kikubwa cha fedha ikiwa imetoa jumla ya pauni milioni 148 kwa usajili wa Maguire uliovunja rekodi, Aaron Wan-Bissaka (pauni milioni 50 kutoka Crystal Palace) na Daniel James (pauni milioni 18 kutoka Swansea).

**Aston Villa**

Klabu iliyopanda daraja ya Aston Villa ikishika nafasi ya pili kwa kutumia kiasi cha pauni milioni 144.5 kwa kusajili wachezaji 12, ambao Tyrone Mings (pauni milioni 26.5), Wesley (pauni milioni 22), Matt Targett (pauni milioni 17) na Douglas Luiz (pauni milioni 15).

**Arsenal**

Imetumia kiasi cha pauni milioni 138, kwa usajili wa Pepe, William Saliba (pauni milioni 27, amepelekwa kwa mkopo St Etienne), Kieran Tierney (pauni milioni 25), David Luiz (pauni milioni 8), Gabriel Martinelli (pauni milioni 6) na Dani Ceballos waliyemchukua kwa mkopo.

**Manchester City**

Walitumia kiasi cha pauni milioni 134.8, wakimchukua kiungo Rodri (pauni milioni 62.5) na beki wa pembeni Joao Cancelo (pauni milioni 60) - pamoja na Zackary Steffen (pauni milioni 7) na Angelino Jose Angel (pauni milioni 5.3).

**Everton**

Wametumia kiasi cha pauni milioni 118.5 kwa kumsajili Alex Iwobi katika siku ya mwisho ya usajili, pamoja na Moise Kean (kwa pauni milioni 27.5), Jean-Phillippe Gbamin (pauni milioni 25), Andre Gomes (pauni milioni 22) na Fabian Delph (pauni milioni 9).

**Tottenham**

Imetumia kiasi cha pauni milioni 100 kwa kumsajili Ryan Sessegnon kutoka Fulham kwa pauni milioni 30 katika saa ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili, wakiwa pia wamemsajili Ndombele na kinda Jack Clarke (pauni milioni 8.5).

**Chelsea**

Licha ya Chelsea kufungiwa kufanya usajili, Blues hao walimchukua moja kwa moja Mateo Kovacic baada ya kucheza kwa mkopo hapo Stamford Bridge.

**Zinginezo**

Leicester wao walitumia pauni milioni 91, wakifuatiwa na West Ham (pauni milioni 78), Newcastle, Wolves (zote zimetumia pauni milioni 65), Brighton (pauni milioni 58.5), Southampton (pauni milioni 50), Bournemouth (pauni milioni 45.7) na Watford (pauni milioni 45.5).

Kwa upande mwingine klabu iliyopanda daraja ya Norwich imetumia kiasi cha pauni milioni 1.1, huku Liverpool (pauni milioni 4.4), Crystal Palace (pauni milioni 11), Burnley (pauni milioni 15), Chelsea (pauni milioni 40), Sheffield United (pauni milioni 43).

**WALIOUZWA**

Kwa pamoja klabu zote za Ligi Kuu zimepata pauni milioni 806.5 kwa kuwauza wachezaji 291.

Chelsea imepata kiasi kikubwa cha pauni milioni 213.2, kwa kuwauza Eden Hazard kwenda Real Madrid kwa pauni milioni 130 na Alvaro Morata kwenda Atletico Madrid kwa pauni milioni 58.3.

Eden Hazard ndiye ameweka rekodi ya kuwa mchezaji ghali zaidi kununuliwa kutoka Ligi Kuu ya England msimu huu.


Leicester baada ya kumuuza Maguire wamepata pauni milioni 80, wakifuatiwa na Manchester United (pauni milioni 74), Everton (pauni milioni 60), Manchester City (pauni milioni 58.1), Arsenal (pauni milioni 55.5), Crystal Palace (pauni milioni 50) na Bournemouth (pauni milioni 36.5).

West Ham (pauni milioni 33.25) na Newcastle (pauni milioni 31.7). Tottenham (pauni milioni 29.7), Liverpool (pauni milioni 28.82), Southampton (pauni milioni 26), Watford (pauni milioni 18.2), Burnley (pauni milioni 8.5) na Wolves (pauni milioni 3).

Katika klabu zote zilizonunua na kuuza wachezaji, imeiacha Aston Villa kuongoza katika chati kwa pauni milioni 144.5, ikifuatiwa na Arsenal (pauni milioni 82.5), Manchester City (pauni milioni 76.7) na Manchester United (pauni milioni 74).

Licha ya kufungiwa Chelsea imepata faida kubwa kwenye usajili ikipata pauni milioni 173.2, huku klabu nyingine tatu zikipata faida, Crystal Palace (pauni milioni 39), Liverpool (pauni milioni 24.4) na Watford (pauni milioni 12.7).

**USILOLIJUA**



KIUNGO mkabaji wa Everton, Morgan Schneiderlin amekuwa mchezaji wa tatu kutolewa kwa kadi nyekundu katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu England kwa klabu hiyo, baada ya Li Tie msimu wa 2003-04 na Phil Jagielka msimu wa 2018-19, lakini pia kutolewa kwake kukiifanya Everton kuwa timu ya kwanza mchezaji wake kulimwa kadi nyekundu tangu ilipotokea kwa Arsenal msimu wa 2010-11 na 2011-12.



# Chalamila amtumia salamu za pole Dk. Kebwe

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ametuma salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Steven Kebwe na familia zilizopoteza ndugu na jamaa katika ajali ya watu kuungua kwa mafuta iliyotokea juzi.

Chalamila alitoa pole hizo juzi wakati wa mkutano na wananchi wa Kata ya Utengule Usongwe, iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kuongoza wakazi hao kusimama kwa dakika moja kuomboleza.

Alisema Mkoa wa Mbeya unaungana na mikoa mingine kuomboleza vifo vya watu zaidi ya 60 waliopoteza maisha baada ya kuungua moto walipokuwa wanachota mafuta baada ya lori lililokuwa limebeba bidhaa hiyo, kuanguka mkoani Morogoro.

Alisema taifa limepoteza Watanzania wengi ambao bado walikuwa wanahitajika na kuwaomba wafiwa wote kujifunga mkanda kwenye kipindi hiki cha majonzi ya kuondokewa na wapendwa wao.

Kutokana na ajali hiyo, Chalamila alipiga marufuku wakazi wa Mbeya kusogelea ajali za malori ya mafuta ili kuchukua bidhaa hiyo kwa sababu ni hatari zinaweza kugharimu maisha yao.

Alisema umekuwa ni utamaduni kwa baadhi ya wananchi hususani madereva bodaboda kukimbilia kuiba mafuta pindi malori yanapoanguka na kusema ni hatari na waache mara moja.

"Tukiwa kwenye maombolezo ya kuwapoteza ndugu zetu waliopoteza maisha baada ya kuungua mafuta, nawasihi wana-Mbeya hususani madereva bodaboda kuacha tabia ya kukimbilia kuiba mafuta kwenye malori yaliyoanguka ili kuokoa maisha yenu," alisema Chalamila.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema taifa limepoteza nguvu kazi ya vijana wengi katika ajali ya moto na kusababisha majeruhi wengi.

Alipongeza jitihada za uokoaji zilizofanywa na Jeshi la Ukoaji na majeshi mengine, madaktari, taasisi na CCM Mkoa wa Morogoro kwa kuhamasisha wananchi kutoa damu kuokoa maisha ya majeruhi.



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, alipokea maelekezo ya namna teknolojia mpya ya kilimo cha mboga kwa kutumia vipando kinavyoweza kumnufaisha mkulima kwa kutumia eneo dogo na kulima mboga mbalimbali na kujiingizia kipato, kwenye Maonyesho ya Wakulima Nanenane jijini Mbeya. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Pinda azitaka taasisi kupambana na udumavu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI Mkuu mstaafu wa Tanzania, Mizengo Pinda (pichani), ameshauri taasisi zinazojihusisha na kilimo na lishe, vyuo na madaktari kuandaa programu maalum ya kutoa elimu kwa jamii hasa kwa wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano kutambua makundi yanayohitajika ili kukabiliana na changamoto ya utapiamlo na udumavu.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akifunga Maonyesho ya Wakulima Nanenane, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini iliyohusisha mikoa saba kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya.

Alisema licha ya mikoa hiyo kuongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, lakini kuna changamoto lishe hali inayosababisha udumavu kwa watoto wanaozaliwa.

Alisema ipo haja ya kuanzisha programu maalum ya kutoa elimu kwa jamii ili kumaliza changamoto ya utapiamlo na udumavu kwa watoto.

"Haiwezekani mikoa hii ya Nyanda za Juu Kusini ikaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara vilevile ikaongoza kwa suala la udumavu ni aibu, lazima tuandae programu maalum ya kuisaidia jamii kuzingatia lishe bora," alisema Pinda.

Pia, aliwashauri kinababa ndani ya familia kuacha ubahiri wa fedha kwa kujitahidi kuwanunulia mahitaji ya nyumbani wake zao.

Alisema wakati wanafikiria kuanzisha programu ya kukabiliana na udumavu pia kinababa wanapaswa kutambua wajibu wao kwa familia ikiwamo kuhudumia.



# Wakulima wa mpunga walia uharibifu wa kweleakwela

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa mpunga katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameomba wataalamu wa kilimo kutafuta mbinu za kisasa kukabiliana na ndege aina ya kweleakwelea ambao kwa sasa ndiyo changamoto kubwa inayowakabili kutokana na kuharibu mazao yao yakiwa shambani.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Mbeya wakati wa kilele Siku ya Maonyesho ya Wakulima Nanenane.

Mmoja wa wakulima hao, Batazan Lusigi, alisema ndege aina ya kweleakwelea wamewasababishia hasara kubwa wakulima wengi kwa sababu huvumia mashamba na kuharibu mazao.

Alisema wataalamu wanapaswa kubuni mbinu za kisasa za kuwadhibiti ndege hao kuokoa mazao shambani yasiharibiwe na ndege hao.

"Msimu wa mavuno ukikaribia ndege hao jamii ya kweleakwelea kwa makundi huvamia mashamba ya wakulima na kuharibu hali inayowasababishia hasara na kushindwa kupata mavuno yanayostahili, tunaomba wataalamu watusaidie suala hili kwa kuwa ni changamoto," alisema Lusigi.

Hata hivyo, Ofisa Kilimo mstaafu, Nuhu Mchame, ambaye kwa sasa anajihusisha na utafiti wa ndege hao, alisema kweleakwelea wanatabia ya kutembea katika makundi makubwa ya ndege zaidi ya milioni moja na wanapoingia shambani husababisha uharibifu mkubwa unaofikia asilimia 75 ya mazao shambani.

Alisema ili kabiliana na uharibifu wa ndege hao lazima itafutwe njia ya kuwadhibiti ikiwamo kuwaua ili wasiendelee kuvamia mashamba ya mpunga na mazao mengine na kuwasababishia hasara wakulima.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema halmashauri yake inashirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Wizara ya Kilimo, kusaidia wakulima kupunguza ndege hao kwa kuwaua kwa kuwamwagia sumu.

Alieleza changamoto kuwa ni ndege hao kujificha na kuzaliana ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ambako sheria hairuhusu kuwaua wakiwa ndani ya hifadhi.

Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune, aliwasihi wakulima kutoa taarifa kwa viongozi wa vijiji na kata wanaobaini makazi ya ndege hao ili wauliwe.

Alikiri ndege hao kuwasababishia hasara kubwa wakulima na kwamba ni rahisi kuhama kwa sababu eneo kubwa linalolimwa mpunga ni tambarare.





# Ndejembi aiagiza Takukuru kuchunguza ujenzi sekondari

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza mradi wa ujenzi wa majengo ya Shule ya Sekondari Kongwa kutokana na kuwapo na harufu ya ubadhirifu wa fedha.

Sambamba na hilo, ameagiza kuhojiwa watumishi wawili wa Halmashauri ya Wilaya hiyo na makandarasi waliokuwa wakijenga majengo hayo kutokana na kukiuka miongozo ya serikali.

Ndejembi alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa majengo hayo.

Aliitaka taasisi hiyo kuchunguza kuanzia manunuzi ya vifaa mpaka bei ya vifaa na maduka yaliyotumika kununua vifaa hivyo, utaratibu wa kupitisha zabuni za ujenzi na thamani halisi ya gharama zilizotumika mpaka kufikia hatua ya majengo hayo.

"Ujenzi huu umekiuka utaratibu na kuisababishia serikali kuingia kwenye hasara kutokana na majengo kutokamilika wakati tayari Sh. milioni 290 zimeshatolewa," alisema.

Alifafanua kuwa serikali ilipeleka Sh. milioni 150 kwa ajili ya mabweni, Sh. milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa bwalo na Sh. milioni 40 kwa ajili ya madarasa na samani zake, lakini baadhi ya majengo hayajakamilika na fedha zimeisha.

Alisema miongozo iliyowekwa na serikali ni kutumia mafundi wa ndani waliopo eneo husika na si kampuni za makandarasi.

Ndejembi alisema tayari Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alishafanya ziara kwenye shule hiyo na kutoa maelekezo kuwa majengo yajengwe kwa kutumia utaratibu wa 'Force account', lakini hawajafuata wataalamu hao.

"Aliagiza kupelekewa taarifa ya ujenzi huu, lakini haijapelekwa jambo ambalo ni dharau haikubaliki, kwa ujumla sijaridhishwa na maendeleo ya ujenzi huu pamoja na thamani halisi ya fedha zilizotumika hapa," alisema.

Aliwataja wanaotakiwa kuhojiwa na Takukuru ni ofisa manunuzi Yunus Mawaka, mhandisi wa ujenzi Wilaya hiyo, Christian Mlay, mkandarasi anayejenga bweni Majuto Mhando na mkandarasi anayejenga bwalo, Alfred Sembisa.

Alisema sababu za kutaka wahusika hao wakamatwe kuwa ni kutokana na kukiuka masharti ya fedha za ujenzi wa majengo hayo na kuwapo na harufu ya ufisadi.

"Hawa wametumia utaratibu wa kushindanisha zabuni kwa makandarasi wakati sisi tunasema tunatumia mafundi waliopo eneo husika ili kupunguza gharama kubwa za ujenzi, wamekiuka masharti," alisema.

Aliutaka uongozi wa halmashauri ya wilaya hiyo kusimamisha kutoa fedha za ujenzi wa majengo hayo zilizobaki kiasi cha Sh. milioni 74 hadi uchunguzi huo utakapokamilika.

Ofisa Elimu Wilaya ya Kongwa, Honorata Kabunduguru, alisema serikali ilipeleka Sh. milioni 290 kwa ajili ya majengo matano ya shule hiyo.

Alisema katika gharama hizo kila jengo lilitakiwa kukamilika pamoja na vifaa vyake mfano mabweni yalitakiwa kukamilika pamoja na kuwekewa samani zake ambazo ni vitanda na magodoro.

Hata hivyo, alisema kabla ya kuhamishiwa wilaya hiyo alikuwa Wilaya ya Mpwapwa ambapo fedha kama hizo zilizotumwa na kukamilisha ujenzi na kununua mahitaji yote kwa kutumia utaratibu wa 'force account' iliyokuwa chini ya kamati za ujenzi za shule husika.



Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi (katikati), akikagua ujenzi wa mradi wa mabweni ya Shule ya Sekondari ya Kongwa mkoani Dodoma, ambapo aliiamuru Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwakamata mhandisi wa ujenzi wa halmashauri hiyo, na ofisa ugavi wa halmashauri hiyo, pamoja na mafundi wawili wa ujenzi huo kutokana na kukiuka masharti ya kutumia fedha hizo, utaratibu ulielekeza kutumia force account na kusababisha majengo hayo kushindwa kukamilika. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Elimu ya stadi za kazi yasisitizwa kwa wafungwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAFUNGWA wametakiwa kuzingatia elimu ya stadi za kazi wanazopewa magerezani ili kujiepusha kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu wanaporudi uraiani.

Wito huo ulitolewa na Kamshina Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini (CGP), Phaustine Kasike, alipotembelea Gereza la Isanga na Msalato jijini hapa kukagua mradi wa ujenzi wa nyumba za maofisa Magereza zinazojengwa kupitia matofali ya kuchoma.

Kasike alisema jeshi hilo lipo kwa ajili ya kurekebisha tabia limekuwa likifundisha wafungwa kazi mbalimbali wakati wakitumikia adhabu zao, ili kuwasaidia kutorudia tabia za uhalifu zilizosababisha kufungwa tena.

Alisema wengi wa wafungwa wamekuwa na uelewa wa kufanya vitu mbalimbali ambapo jeshi hilo linawaendeleza ili wakitoka wakaendeleze ujuzi walioupata badala ya kufanya uhalifu kama walivyokuwa awali.

"Naomba mzingatie mafunzo ya stadi za kazi mnayopewa mkiwa gerezani ili mkitoka mkayafanyie kazi ambapo yatawasaidia kuwaingizia kipato," alisema.

Alibainisha kuwa hakuna sababu ya wao kurudia makosa waliyofanya kwa kuwa wamepata mafunzo ya stadi za kazi ambayo yatakuwa silaha kubwa mkiwa uraiani.

"Mmefundishwa ujenzi, ufyatuaji matofali, ufundi selemala na fani nyingine nyingi jambo ambalo mkizingatia litawaepushia kufanya uhalifu kwa mara nyingine kipindi mtakapomaliza adhabu zenu," alisema. Akizungumzia kuhusu matofali hayo, alisema jamii haijui kuhusu matofali ya kuchomwa na pumba na kuwataka wao wakawe mabalozi wa kutoa elimu hiyo wakitoka uraiani ambayo itasaidia kuondokana na uharibifu wa mazingira.

Mfungwa Aman Nikohed, alisema yeye ni fundi ujenzi mzuri na amekuwa akiwafundishwa wenzie fani hiyo kupitia ujenzi wanaofanya kwenye nyumba hizo.

Alisema wana kila sababu ya kujivunia fursa wanayopewa na jeshi hilo kuendeleza fani zao pamoja na kuwa wanatumikia adhabu kutokana na makosa waliokutwa nayo. Naye Nicholas Cosam alisema wakati anaingia gerezani alikuwa hajui kitu chochote kuhusu ufundi wala ufyatuaji matofali, lakini amefanikiwa kupata ujuzi huo na ataendelea kujifunza ili akitoka uraiani akautumie kwa ajili ya kujiingizia kipato.

## Kituo maalum chatakiwa kwa kukusanya asali

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

SERIKALI imeombwa kuwatafutia wavuna asali kituo maalumu cha ukusanyaji zao hilo kutoka mashambani ili iwe rahisi kuwabaini baadhi ya watu wanaochakachua asali kabla haijaingia sokoni.

Akizungumza na Nipashe katika viwanja vya Nanenane, mjasiriamali Christina Mushi, alisema ni muhimu serikali kuwa na kituo maalumu cha kukusanyia asali zao kwa ajili ya kuiuza kwa wafanyabiashara ili kuondokana na tabia ya baadhi ya watu kuchakachua na kuifanya asali kukosa viwango.

Aidha, alisema itawasaidia kwa kiasi kikubwa kukuza soko la bidhaa hiyo ndani na nje ya nchi kwa kuwa itapatikana asali yenye ubora.

"Kikiwapo kituo maalum ambacho kitakuwa kikipima kiwango na ubora wa asali hakuna atakayethubutu kuchakachua na badala yake italetwa asali iliyobora ambayo itapata soko kwa haraka," alisema.

Alisema bila kufanya hivyo watu wachache wataendelea kuharibu zao hilo kutokana na tamaa ili wapate asali nyingi.

"Tunaiomba serikali ifanye jitihada ya kuanzisha kituo hiko tunahitaji kuingia katika soko la ushindani kwenye zao la asali kimataifa," alisema Christina.

Alifafanua zaidi ya kuwa hivi sasa ni vigumu kupata asali inayofanana kwa sababu kila mmoja anakusanya asali kivyake na kuileta sokoni jambo ambalo sio rahisi kuwabaini wanaochakachua.

Kadhalika, alilishukuru Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani Dodoma ambao wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha inawafundisha wajasiriamali kutengeneza bidhaa zenye ubora unaotakiwa sokoni.

Aliwaasa wajasiriamali jijini Dodoma kujitokeza katika mafunzo yanayotolewa na shirika hilo ili wapate ujuzi ambao utawasaidia kuingiza bidhaa zao katika soko la kimataifa badala ya kuziuza mtaani pekee.

Naye mjasiriamali Hagai Wille, alisema hivi sasa vikundi vya wajasiriamali vinapaswa kujitoa kwenda kupata mafunzo yatakayowasaidia kukuza biashara zao.

# Aagiza kuwekwa michoro ya zebra barabarani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani ambaye pia ni Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, amezitaka mamlaka husika kuweka michoro ya alama za barabarani (zebra) ili kuondoa usumbufu wanaoupata watumiaji wa barabara.

Aliyasema hayo Mjini Zanzibar wakati Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na Bodi ya Usafiri Zanzibar zilipofanya operesheni ya usalama barabarani.

"Naomba nitoe angalizo kwa wake wote ambao wanapewa kazi ya kuweka michoro barabarani waweke kwa kutumia rangi ambayo inastahili na nzuri inayokaa barabarani kwa muda mrefu zaidi," alisema.

Vile vile, aliitaka mamlaka inayohusika na uwekaji wa alama barabarani kuzirudishia alama hizo zilizofutika mara moja kwa kuwa kuziacha hivyo kutasababisha ajali.

Naye Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Injinia Hamad Yusuf Masauni, alisema kupitia operesheni hiyo wamegundua changamoto mbalimbali na kuahidi kuzifanyia kazi.

Alisema, kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi ya shida ambazo wanazipata wakitumia vyombo vya usafiri kwenda katika shughuli zao za kila siku.

Alieleza kuwa katika maeneo ya mjini kuna shule nyingi za sekondari na elimu ya juu hivyo wanafunzi ambao wanasoma katika shule hizo wengi wao wanakaa nje ya mji na kupata tabu ya usafiri kurudi majumbani kwao.

"Wale wanafunzi ambao wanajiandaa kwa mitihani ya kidato cha nne na sita wakati mwingine utakuta changamoto ya kutokufanya vizuri katika masomo yao inachangia na usumbufu wanaoupata njiani ikiwa pamoja na kusumbuliwa kwa madereva kugoma kuwachukua," alisema.

Alivitaka vyombo vya usalama likiwamo Jeshi la Polisi kwa upande wa usalama barabarani kuhakikisha wanashirikiana na Bodi ya Usafiri Zanzibar kudhibiti matukio kama hayo yasijitokeze ili wananchi wasiendelee kupata usumbufu wa aina yoyote.

Masauni pia aliwataka askari wa usalama barabarani ambao wanawabambikizia kesi madereva kuacha.

Kwa upande wake Katibu wa Bodi ya Usalama Barabarani, Mohammed Simba, aliwataka madereva wa gari za abiria kuacha kuwanyanyasa wanafunzi wakati wanapohitaji usafiri huo.

Pia aliwataka wananchi watakapokutana na tatizo lolote linalohusiana na sekta ya usafiri barabarani, warekodi nambari ya gari na wapeleke katika idara ya leseni na usafirishaji ili wachukuliwa hatua.

Kwa upande wao madereva wanaofanya safari zao katika maeneo tofauti ya Unguja wamesema changamoto ambazo zinawakabili ni pamoja na kufutika kwa alama za barabarani pamoja na kutokuwapo kwa vituo maalum vya daladala.

# Balozi Iddi apongeza ujio madaktari bingwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema msaada mkubwa unaoendelea kutolewa na Madaktari Mabingwa wa Afya kutoka Chuo Kikuu cha Alexandria nchini Misri, unazidi kuleta faraja kwa wananchi wengi visiwani Zanzibar.

Alisema familia kadhaa zilizowahi na zinazoendelea kupata huduma za upasuaji kwa wagonjwa wao kupitia madaktari hao wa Misri wanaokuja visiwani humo kwa vipindi tofauti tangu mwaka 2013, zimejenga matumaini makubwa ya kuimarika kwa afya za wagonjwa wao.

Aliyasema hayo ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar wakati akizungumza na timu ya madaktari mabingwa kutoka Chuo Kikuu cha Alexandria, nchini Misri waliowasili Zanzibar kufanya upasuaji kwa wagonjwa 66 waliozaliwa na maradhi yasiyo ya kawaida.

Alisema ujio wa timu hiyo ya wataalamu wa afya kwa upande mwingine mbali ya kutoa huduma za afya, lakini pia utaongeza fursa za utaalamu kwa madaktari wazalendo waliopo hapa nchini.

Pia, aliushauri na kuuomba uongozi wa Chuo Kikuu cha Alexandria kuendelea kutoa nafasi zaidi za mafunzo ya juu kwa madaktari wazalendo wa Zanzibar kwenye vyuo vikuu mbalimbali nchini Misri, taifa ambalo limepiga hatua kubwa katika taaluma ya afya.

Naye kiongozi wa timu ya madaktari hao, Profesa Sabri Wahid, alisema operesheni 350 tayari zimeshafanyika kupitia mfumo huo wa uwekaji kambi ikiwa ni mara ya sita tangu ulipoanzishwa mwaka 2013.

Profesa Sabri alisema operesheni za kambi ya mwaka huu zinahusisha watoto wapatao 52 na watu wazima 14 waliozaliwa na matatizo yasiyo ya kawaida katika maumbile ya mwanaadamu.

Alisema uamuzi wa uongozi wa chuo hicho wa kuweka kambi umekuja katika azma ya kuendeleza ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kupunguza gharama kubwa za matibabu ambazo zingeigharimu serikali katika kuwahudumia wananchi wake.

Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohamed, alisema serikali kupitia wizara anayoisimamia inaendelea kujenga miundombinu imara katika sekta ya afya hasa majengo kiasi ambayo Misri ina fursa ya kuendelea kusaidia utaalamu katika sekta hiyo.

Hamad alisema hospitali nyingi kubwa bado hazijatosheleza watendaji wenye uwezo mkubwa unaolingana na hospitali hizo zinazolenga kutoa huduma za afya katika muda wote.



Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Sira Ubwa Mamboya (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo na kuangalia gari lenye mtambo maalum (halipo pichani) huku wakufuatilia matumizi ya masafa kutoka kwa mtaalamu wa TCRA wakati wa ziara yake kwenye taasisi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA** WETU

# Mama aliyetupa mtoto na kuokolewa na mbwa kukiona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, imesema itamchukulia hatua mama aliyemtupa mtoto wake baada ya kumzaa ambaye aliokolewa na mbwa huko kisiwani Pemba.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Shadya Mohammed Suleiman, amewashauri wazazi ambao bado hawajawa tayari kuzaa, kutumia njia za uzazi wa mpango kuliko kuzaa na kuwatupa watoto.

Tukio la kusikitisha lilitokea Agosti 7, mwaka huu huko Pujini Pemba, baada ya mtoto mchanga kutupwa na mama yake na kisha kuokolewa na mbwa. Alikuwa akizungumza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, wakati akimpokea mtoto huyo ambaye aliyepokelewa na kituo cha kulelea watoto yatima Mazizini.

Alisema ikiwa wanawake wanajihisi bado ni vijana basi waende hospitali kwa ajili ya kujiunga na uzazi wa mpango kwa kuwa huduma hizo zinatolewa bila ya malipo.

"Tumewekewa njia tofauti za kujikinga kupata mimba kuliko kitendo hichi alichokifanya mwanamke mwenzetu, hakifanani na sio kitendo cha kibinadamu kuzaa mtoto ukamtupa akaokolewa na mnyama ambaye ana akili tofauti na sisi binadamu, tunakilaani sana kitendo hichi," alisema.

Alisema, kitendo kilichofanywa na mama mzazi wa mtoto huyo ni cha kulaaniwa kwa kuwa mtoto huyo hana hatia.

Alisema wizara itahakikisha inamchukulia hatua mama mzazi wa mtoto huyo ikiwamo kufikishwa mahakamani.

"Tumeshirikiana na Jeshi la Polisi tayari mama mzazi ameshapatikana, lakini kutokana na hali yake amepewa dhamana na anatakiwa kupewa huduma kama mzazi ambaye amejifungua na baadaye taratibu za kisheria zitafuata," alisisitiza. Alisema mbwa aliyemwokoa mtoto huyo angekuwa anafugwa katika nyumba maalum basi angezawadiwa zawadi, lakini haiwezekani kwa sababu mbwa huyo anaishi msituni.

Aliwasisitiza kinamama kuacha kuwafanyia ukatili watoto na badala yake kuwapeleka katika nyumba maalum zilizowekwa na serikali kwa ajili ya kuwatunza watoto.

Kwa upande wake mlezi mkuu wa nyumba ya kulelea watoto yatima Mazizini, Chum Ali Abeid, aliyekabidhiwa mtoto huyo, aliahidi kumlea kwa moyo wa upendo na huruma kama watoto wengine ambao wanapata malezi katika nyumba hiyo.

Mtoto huyo alifikishwa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja kwa ajili ya kuchunguzwa afya yake na hali yake inaendelea vizuri.

Mama mzazi wa mtoto huyo alitambulika kwa jina la Khadija Hamad Ali (30) na alijifungua mtoto huyo majira ya 10:30 usiku Agosti 7, katika msitu na kuamua kumtelekeza mtoto wake kwa kumtupa.

# SADC yaviamsha viwanda vya Tanzania kujikita masoko nje

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

MKUTANO wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) umeamsha ari ya viwanda vya Tanzania kupanua wigo wa kibiashara kwa kuongeza uzalishaji ili bidhaa za ndani na kutafuta masoko katika nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki, baada ya ujumbe wa SADC uliopo nchini, kufanya ziara katika kiwanda cha kutengeneza vifungashio cha Global Packaging Limited kilhoko Kibaha, mkoani Pwani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Global Packaging (T) Limited, Benno Mwitumba, alisema kiwanda chake kimepanga kupanua wigo wa uzalishaji kwa kuanzisha awamu nyingine ya upanuzi wa kiwanda kwa lengo la kuongeza uzalishaji, hukumasoko yakitafutwa zaidi kwenye nchi nyingine za SADC. Mwitumba amesema kiwanda hicho ambacho kilizinduliwa na Rais

John Magufuli Juni mwaka 2017, kimesaidia kwa kiwango kikubwa kuongeza uzalishaji wa vifungashio kukidhi soko la ndani, na sasa mkakati ni kukipanua kiwanda pamoja na uzalishaji ili kuweza kukidhi mahitaji ya soko katika nchi za SADC.

"Miaka hii miwili tumepata mafanikio makubwa na uzalishaji na tunataka kuingia katika awamu ya tatu ya upanuzi wa kiwanda chetu baada ya kupata hamasa kubwa ya uwapo wa soko kwenye nchi wanachama wa SADC," alisema Mwitumba.

Alisisitiza: "Tunakusudia kwamba baada ya kukamilisha upanuzi huo,

tutaweza kuuza vifungashio hivi nje na hasa tukiliwania zaidi soko lililopo kwa wenzetu ndani ya SADC, na kwa msaada wa serikali yetu tunaamini azma yetu itatimia."

Aliziomba taasisi za serikali zinazohusika katika uwekezaji, kutoa huduma kwa haraka pasipo urasimu kwa wawekezaji, ili jitihada za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda iweze kukamilika kama ilivyokusudiwa na serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Prof. Damian Gabagambi, alisema NDC kama mwanahisa kwenye kiwanda hicho cha Global Packaging Limited, inaona fursa kubwa iliyopo

ya masoko katika nchi za SADC, na hivyo itahakikisha azma ya upanuzi

inafanikiwa na soko la uhakika kutafuntwa kwenye nchi hizo.

"Kwa sasa uzalishaji wetu ni vifungashio vidogo milioni 25 kwa mwaka ama vikubwa milioni 17, tunakusudia upanuzi wa kiwanda utasaidia kuongeza uzalishaji mara tatu zaidi, na hivyo kupenya kwa nguvu zote katika soko la nchi za SADC," alisema Prof. Gabagambi.

Naye kiongozi wa ujumbe wa SADC uliyotembelea kiwanda hicho, Gastom Kaziri, alikipongeza kiwanda hicho kwa kuwa na teknolojia ya hali ya juu, ambayo inafanya kiwanda kizalishe vifungashio vingi kwa muda mfupi, huku vikiwa na ubora wa kimataifa.

"Global Packaging ni mfano wa kampuni zinazotumia teknolojia kubwa, na kwa hatua mliyofikia sasa, ni vema mkatoka nje ya Tanzania hata ikibidi kujenga viwanda nje ama kutafuta masoko ya bidhaa zenu huko nje ya nchi," alisema Bwana Kaziri.

Mmiliki wa Wande Printing and Packaging (T) Ltd ambao ni wanahisa katika kampuni ya Global Packaging (T) Ltd, Joseph Wasonga, alielezea harakati za upanuzi wa kiwanda zinakwenda vizuri, huku akipongeza ushiriki wa taasisi za kifedha katika kufanikisha jitihada za ujenzi wa Tanzania ya viwanda.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, akiangalia zizi la mbuzi la mmoja wa wanufaika wa Tasaf, Beatha Katushabe wa kijiji cha Rulalo wilayani Karagwe mkoani Kagera, ambaye anamiliki mbuzi 25 aliowapata kutokana na ruzuku ya mpango wa kunusuru kaya maskini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibano watupa taka holela chaja

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

SERIKALI imezitaka halmashauri zote nchini kutenga maeneo maalum mbali na makazi ya watu yatakayotumika kujenga madampo ya kisasa ili kuzingatia hifadhi ya mazingira.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa dampo la kisasa linalojengwa eneo la Buhongwa jijini Mwanza.

Alisema ujenzi huo wa dampo la kisasa utasaidia juhudi za serikali za kutotumia fedha nyingi kwenye ununuzi wa vifaa tiba kwa kuwa taka zitakazolishwa katika Jiji la Mwanza zitapelekwa dampo kwa wakati na kunusuru magonjwa ya mlipuko.

"Huwezi kutenganisha afya na mazingira, mradi huu ni mkubwa sana na kwa namna utakavyotekelezwa hatutarajii kuona taka mjini zinazagaa. Tunatarajia kuona taka zote zinakuja hapa," Sima alisema.

"Natoa rai kwa halmashauri zingine ambazo zinatekeleza miradi ya kimkakati kutoa kipaumbele kwa ujenzi wa madampo ya kisasa na kuchukua hatua dhidi ya wachafuzi wa mazingira," aliagiza.

Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Kiomoni Kibamba, alibainisha kuwa dampo hilo lina ukubwa wa hekta 34 na linatarajia kukamilika Desemba mwaka huu na kwa sasa ujenzi upo asilimia 78 ukigharimu Sh. bilioni 16.6, ukienda sambamba na ujenzi wa barabara.

"Dampo hilo litakuwa na chemba sita za kuhifadhi taka na mabwawa ya kuhifadhi majitaka, barabara za kisasa zenye urefu wa kilomita 1.9, taa za nishati ya jua na maabara maalum ya kupima majitaka," Kibamba alifafanua.

Alisema kukamilika kwa dampo hilo la kisasa mbali na kuwezesha uteketezaji wa taka jijini mara baada ya kufikishwa kwenye eneo hilo, kutaongeza mapato katika jiji hilo.

Kwa mujibu wa Kibamba, tani 33 hadi 36 zinatarajia kupelekwa katika dampo hilo mara baada ya ujenzi kukamilika na linatarajia kudumu kwa zaidi ya miaka 15.

# Mradi mkubwa wa maji bil.70/- waja

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maji na Umwagiliaji, Profesa Makame Mbarawa, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika sherehe za uwekaji saini wa mradi mkubwa wa maji ambao unaanzia Mugango, Kiabakari hadi Butiama mkoani Mara.

Tukio hilo la kuweka saini litafanyika Agosti 15, mwaka huu, kijijini Mugango ambako kuna mitambo ya maji kutoka Ziwa Victoria ambako litawekwa bomba jipya la maji.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu jana kuwa gharama la mradi huo ni Dola za Kimarekani 30.69, ambazo ni sawa na Sh. bilioni 70 za Kitanzania.

"Prof. Mbarawa atakuwa mgeni rasmi utiaji saini mkataba wa mkandarasi wa ujenzi wa mradi mpya wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyasambaza maeneo ya Wilaya ya Musoma Vijijini na Butiama," alisema Dk. Anney.

Mkuu huyo wa wilaya alisema mradi huo unafadhiliwa na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (Badea), Serikali ya Saudi Arabia na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili kuwezesha wakazi wa Musoma Vijijini na Butiama kupata maji ya uhakika.

"Ninayo furaha kuwaalika Watanzania wote kwenye hafla ya utiaji saini, katika tukio hili muhimu na kubwa litafanyika kijijini Mugango, ambako mradi huo unaanzia na kuelekea Kiabakari hadi Butiama," alisema.

Dk. Anne alifafanua kuwa mradi huo utakapokamilika unatarajia kunufaisha wananchi 80,000 vikiwamo vijiji 13, ambavyo vipo kilometa 12 kutoka lilipo bomba kuu za kusambaza maji.

Alisema mbali na mradi huo mkubwa, kuna miradi mingine ya maji imekuwa ikiendelea Musoma Vijijini ikilenga kusogeza huduma za maji karibu na wananchi na kuwaondolea usumbufu wa kutembea umbali mrefu.

"Kwa mfano upo mradi wa kusambaza maji katika vijiji vya Bulinga, Bujaga, Bukima, Busungu, Rusoli, Kwikerege na vingine vingi ambao unaendelea vizuri kwani kuna tangi kubwa limejengwa la kusambaza maji hayo," alisema.

## Wanaotaka kujitenga Yemen waudhibiti mji wa Aden

**SANA'A, Yemen**

MAOFISA usalama wa Yemen wamesema wananchi wanaotaka kujitenga Yemen wamepata udhibiti wa mji wa bandari wa Aden.

Wamesema watu hao wamekuwa wakiungwa mkono na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), wamekuwa wakipigana kama sehemu ya muungano unaoongozwa na Saudi Arabia ambao unaunga mkono serikali.

Maofisa hao wamesema kuwa waliofariki katika mapigano yaliyodumu kwa siku nne imeongezeka na kufikia watu 70, ikiwa ni pamoja na raia.

Imeelezwa kuwa matukio yaliyotokea hivi karibuni yanaweza kuvuruga zaidi muungano huo ambao umekuwa ukipambana na waasi wa Kihouthi ambao ni washirika wa Iran tangu mwaka 2015 kwa niaba ya serikali ya Rais Abed Rabbo Mansour.

Msemaji wa muungano unaoongozwa na Saudi Arabia, Kanali Turki al-Maliki, alinukuliwa jana katika Shirika la Serikali ya Saudia akisema kuwa: "Uongozi wa pamoja wa muungano unatoa wito wa kusitishwa mara moja mapigano katika mji mkuu wa mpito wa Yemen, Aden na utatumia nguvu za kijeshi dhidi ya wale watakaokiuka hatua hiyo."

Alisema muungano huo wa kijeshi unatoa wito kwa Baraza la Mpito la wanaotaka kujitenga upande wa kusini pamoja na majeshi ya ukanda wa usalama kurejea mara moja katika maeneo yao, kujiondoa kutoka katika maeneo yote waliyoyakamata katika muda wa siku chache zilizopita.

**DW**

# Maelfu waandamana Mashariki ya Congo

**KINSHASA, Congo**

WAANDAMANAJI wapatao 5,000 jana walifunga barabara za mji wa Beni Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) pamoja na kuchoma moto matairi.

Waandamanji hao walikuwa wakipinga mauaji yanayofanyika katika eneo hilo, ikiwamo vifo sita vilivyotokea katika kipindi cha saa 24 zilizopita kabla ya kutokea kwa maandamano hayo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi, Kanali Safari Kazingufu alisema maofisa wa polisi waliwatawanya watu na kusafisha barabara kuu za mji huo baada ya waandamanaji kuweka vizuizi katika barabara hizo kuanzia saa 12:30 asubuhi.

Maandamano kama hayo yalifanyika Jumatano ya wiki iliyopita ambapo waandamanaji walitembea umbali wa kilomita 15 kuwasilisha barua katika Ofisi ya Tume ya kulinda amani ya Umoja wa Mataifa, (MONUSCO), katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Vikundi kadhaa vyenye silaha likiwamo kundi la Allied Democratic Forces, (ADF), pamoja na magenge ya wahalifu yanafanya mashambulizi katika mji huo wa Beni na Jimbo la Kivu Kaskazini, ili kulidhibiti eneo hilo lenye utajiri wa madini.

**DW**



Waandamanaji nchini Congo wakiwa wamefunga barabara za mji wa Beni pamoja na kuchoma moto matairi jana wakipinga mauaji yanayofanyika katika eneo hilo. **PICHA: REUTERS**

## Alidumbukiza mtoni gari alilozawadiwa

**NEW DELHI, India**

RAIA mmoja wa India amelidumbukiza mtoni gari aina ya BWM alilozawadiwa wakati akisherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Mashuhuda wa tukio hilo wameeleza kuwa, mtu huyo aliamua kufanya kitendo hicho baada ya kupewa zawadi ambayo hakuitaka.

Imeelezwa kuwa mtu aliahidiwa zaidi ya gari aina ya Jaguar na mpenzi wake, lakini alishangaa analetewa gari aina ya BMW.

Kanda ya video iliochapishwa katika mitandao ya kijamii iliionyesha gari hilo likielea katika mto huo katika jimbo la kaskazini mwa India la Haryana.

Gari hilo baadaye lilisukumwa hadi katika kingo za mto huo na mwanamume huyo anayedaiwa kuwa mwana wa mmiliki wa nyumba kadhaa katika eneo hilo akajaribu kuliokoa.

Maofisa wa polisi wanachunguza kisa hicho, kulingana na vyombo vya habari vya eneo hilo. Gari la BMW linagharimu zaidi ya 3.5m rupees { $49,000} nchini India huku lile la Jaguar likigharimu 4-5m rupees.

**BBC**

## Waziri wa Mambo ya Nje wa India azuru China

**BEIJING, China**

WAZIRI wa Mambo ya Nje India, Subrahmanyam Jaishankar amekwenda China katika muktadha wa mgogoro wa Jimbo la Kashmir, kwamba sehemu kubwa ya mazungumzo anayotarajiwa kufanya na wenyeji wake yatahusu mgogoro huo.

Lengo la ziara ya waziri huyo nchini China ni kupunguza mivutano na nchi hiyo baada ya uamuzi wa serikali ya India juu ya jimbo hilo linaloitwa Jammuna Kashmir.

Jimbo la Kashmir limegawika katika sehemu mbili zinazosimamiwa na India na Pakistan na kila upande unadai umiliki wa jimbo lote peke yake.

Eneo hilo limekuwa la mzozo tangu nchi hizo zipate uhuru mnamo mwaka 1947.

India inamiliki asilimia 45 ya Jimbo la Kashmir wakati Pakistan inasimamia asilimia 35 ya sehemu hiyo na asilimia 20 ya jimbo hilo inadhibitiwa na China.

China imekuwa inapinga sera ya India ya kuiweka sehemu yake ya upande wa magharibi wa mpaka wa nchi mbili hizo chini ya utawala wa India.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Hua Chunying ameeleza kuwa India imeamua peke yake kuyahujumu mamlaka ya China kwa kuibadilisha sheria yake juu ya Kashmir.

Msemaji huyo, ameongeza kwa kusema kwamba hatua iliyochukuliwa na India haikubaliki na kwamba haitakuwa na tija kisheria.

India na China ni nchi zenye idadi kubwa ya watu duniani, zimekuwa zinazozana juu ya migogoro ya mipaka isiyokuwa na usuluhisho.

China inadai eneo la kilometa za mraba 90,000 katika Jimbo la India la Arunachal Pradesh. Sehemu hiyo inaitwa Tibet ya Kusini na China.

Kwa upande wake India inadai sehemu ya milima ya Aksai China yenye ukubwa wa kilomita za mraba 38,000.

Jaishankar amekwenda China baada ya Waziri wa Mambo ya Nje wa Pakistan, Shah Mahmood Qureshi kufanya ziara katika nchi hiyo.

Kwa upande wake India imeeleza kwamba uamuzi wake juu ya Kashmir ni suala la ndani ya nchi hiyo na kwamba imechukua uamuzi huo katika juhudi za kukomesha ugaidi kwenye jimbo hilo na pia kuwazuia wanaotaka kujitenga.

**DW**

# Mbunge aandaa hoja binafsi kutetea wenye ulemavu

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Ubungo, Saed Kubenea, amesema anakusudia kupeleka bungeni hoja binafsi ya kuitaka serikali kupeleka bungeni hati ya kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu haki za watu wenye ulemavu wa Afrika uliopitishwa na wakuu wa nchi za Afrika Januari 29 mwaka jana.

Akizungumza na wanahabari jana jijini Dar es Salaam, aliitaka kufanyia marekebisho sera ya watu wenye ualbino nchini inayotumika sasa ili iweze kukidhi mahitaji ya makundi yote ikiwamo kuwapa upendeleo maalum watu wenye ualbino.

Kubenea alisema ingawa zipo sheria na sera mbalimbali zinazozungumzia watu wenye ulemavu, lakini kwa mazingira ya sasa ipo haja ya sera hizo kupitiwa upya ili kuendana na mazingira ya sasa ambayo ni hatarishi kwa watu wenye ualbino.

Akitaja mifano mbalimbali ya matukio yanayowakabili watu wenye ualbino ikiwamo kufukuliwa kwa makaburi yao na matukio ya kutekwa na kukatwa viungo vyao, huku akiitaka jamii kuachana na imani potofu ya kutaka kufikia mafanikio kupitia viungo vya watu wenye ulemavu.

Katika kumuenzi aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, marehemu Dk. Reginald Mengi, mbunge huyo amewataka wanahabari pamoja na wananchi kumuenzi kwa vitendo kwa kuwajali watu wote wenye ulemavu ili kudumisha amani na mshikamano wa jamii.

"Mkuu wa Mkoa (Paul) Makonda alisema nina deni la kulipa kwa mzee Mengi, deni lenyewe ndio hili la kuwakumbuka watu wenye ulemavu kama ambavyo yeye alifanya," Kubenea alisema.

Akizungumza katika mkutano huo mwanasheria wa shirika lianalosaidia watu wenye ulemavu nchini la Under The Same Sun, Maduhu William, aliwaomba wabunge kuiunga mkono hoja hio binafsi ya Kubenea bila kujali utofauti wa vyama kwa kuwa ina lengo jema la kuwasaidia watu wenye ulemavu.

"Mheshimiwa Kubenea atakapopeleka hii hoja bungeni, tunaamini kwamba atapata sapoti ya wabunge wa pande zote mbili tukiamini kwamba wao pia ni sehemu ya jamii, na tutashangaa sana kama tutaona kuna wabunge watapinga hoja hii kwa sababu inagusa maslahi ya Watanzania wenzao," Maduhu alisema.

# JPM: TUSIHUKUMU

INATOKA UK. 3

Hospitali ya Rufani Morogoro inaweza kuwahudumia," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Profesa Lawrence Museru, alisema wagonjwa 43 mahitaji yao ni mengi kwa kuwa wamepata majeraha makubwa ya moto.

Alisema hospitali itatoa huduma zote muhimu kwa majeruhi wawili ambao wameumia kwa asilimia 95 hadi 100.

"Tunawafanyakazi kutoka jeshi, madaktari wetu, tuna wauguzi 60 na tumepata wanafunzi manesi kutoka Muhas, imesaidia sana kuhakikisha huduma sahihi zinafanyika kwa majeruhi," alisema.

**JPM WODINI**

"Poleni sana tunawashukuru kwa yote mnayoyafanya, Mungu awajalie, tuendelee kuwaombea kwa mwenyezi Mungu," alisema Rais.

Aliwatembelea wagonjwa watatu waliounguа kwa asilimia 90 hadi 95, waliolazwa katika chumba cha wagonjwa mahututi.

Mgonjwa mmoja ameungua kwa asilimia 95 na kubaki sehemu ya kichwa na mwingine ameungua sehemu za mapafu.

"Tunawashukuru sana kwa huduma mnazozitoa, Mungu aendelee kuwajalia, na awajalie uponyaji wagonjwa wote," alisema.

Akiwa kwenye wodi ya Sewahaji, alimtembelea mgonjwa Lucas na kumwambia: "Mimi nimekuja kukusalimu, Mungu akusaidie Lucas, pole sana! Nashukuru baba yangu, Mungu akubariki," alisema na kisha kumpa Sh. 500,000.



Naye, Rajabu Mtita ambaye alisema alikuwa mpita njia kwenye eneo la tukio na moto kumfuata, alitumia dakika chache kumsifia rais kuwa anamwelewa na kumkubali.

**MGONJWA AOMBA KITAMBULISHO**

Mtita alitumia fursa hiyo ya kuongeza na rais kwa kueleza suala la upatikanaji wa vitambulisho vya uraia lilivyo gumu na rais alimtaka apone kwanza ndiyo atashughulikia suala hilo.

**DEREVA ALIYEUNGUA**

Rais Magufuli pia alimtembelea Shaban Maliganya, ambaye alijitambulisha kuwa ni dereva wa lori, aliyekwenda kwenye gari lililoanguka kwa ajili ya kutoa msaada na moto kulipuka.

**MAMA LISHE**

Alipofika katika kitanda cha Asha Suleiman, ambaye ni mama lishe kwenye eneo hilo la ajali, Rais Magufuli alimpa Sh. 500,000.

Mama huyo alishukuru huku akilia na kusema amekuwa akimtazama rais kwenye runinga.

Rais alimfariji na kumwambia Mungu ni mwema atamsimamia na atapona.

"Hii hapa itakusaidia nawe hata kununua juisi. Itakusaidia hii hapa Sh. 500,000," alisema wakati akitoa fedha kwa kila mgonjwa.

Pia, aliwapa madaktari na manesi wa wodi ya Sewahaji Sh. 500,000 na wodi ya wanawake Sh. milioni moja.

Katika wodi ya Mwaisela rais alipewa maelezo kuwa wamepokea wagonjwa 10 wanaume wenye miaka 26 hadi 50 ambao wanahitaji kupumua kwa mashine na watatu wanatumia Oxygen.

Alijulishwa kuwa hali za wagonjwa hao ni mbaya kwa kuwa wengi wameungua kwa asilimia 80 hadi 90 kwenye njia ya hewa na chakula hali inayowafanya washindwe kupumua.

Akiwa mwenye huzuni rais alitoa Sh. milioni moja kwa ajili ya kuwahudumia wagonjwa wa 11 waliokuwapo na Sh. milioni mbili kwa ajili ya wauguzi, manesi na madaktari huku akisisitiza kuwa hajawahonga fedha hizo.

# Serikali yaunda tume, majeruhi wafikia 71

INATOKA UK. 3

"Kabla ya aliyechomoa betri tumeona wanaokuja na kuondoka wanachota na kuchota wanaondoka, nani aliwazuia? Alihoji huku wananchi wakijibu "hakuna".

Alisema je, Kikosi cha Zimamoto ambacho kilikwenda baadaye kuzima moto huo, itachunguzwa kama walifika kwa wakati na kuzima moto huo.

"Tumesisitiza umakini katika utendaji ndani ya serikali, tumesisitiza umakini mahali pa kazi na uwajibikaji, kama serikali hatujawajibika nataka tujue, tunaambiwa tuliokoa mafuta, nataka kujua tuliokoa mafuta yakiwa yameisha kuungua?" Alisema na kuongeza:

"Na sisi serikali lazima tujiridhishe ndani ya serikali kama tuliwajibika vizuri, sababu ajali hii imetokea katikati ya manispaa, tena saa mbili asubuhi watu wanafanya kazi, je, wakati ajali inatokea kila mmoja aliwajibika ipasavyo, ilivyoanguka tu nani alijitokeza kwanza?"

"Aliyezima moto ni 'fire' (zima moto) aliokoa mafuta au maji yaliyomwagwa, kuna vitu lazima tuviangalie tujue nani alihusika." Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, serikali haitaacha jambo hilo likapita lilivyo bali hatua zitachukuliwa kwa ambao walishindwa kuwajibika ipasavyo.

Ataka wananchi kuchukua tahadhari

"Ajali za namna hii siyo za mara ya kwanza ilitokea Mbalizi mkoani Mbeya, nawasihi sana Watanzania iwe gari kubwa au dogo linapoanguka msitumie nafasi hiyo kama fursa nendeni mkaokoe binadamu aliyepo pale na si vinginevyo," alitahadharisha.

Alisema ni vyema watu wakashiriki kuokoa watu na siyo kukimbilia vitu, na kwamba ajali hiyo imeacha fundisho kubwa kwa Watanzania.

**SERIKALI KUZIKA MIILI**

Aidha, alisema serikali itasimamia mazishi kwa miili yote iliyotambulika ambayo itazikwa katika makaburi ya Kola, na kwamba ndugu watakaokuwa tayari kuchukua miili ya ndugu zao kwenda kuzika wenyewe kwenye makaburi ambayo yameshaandaliwa wataruhusiwa.

Waziri Mkuu alisema kwa ambao watashindwa kuwatambua ndugu zao kutokana na kuungua vibaya, serikali itasimamia upimaji wa vinasaba (DNA) baina ya ndugu na miili ili kuhakikisha wanawatambua ndugu zao na kwamba upimaji umeshaanza utaendelea hadi leo.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi ofisi ya Waziri Mkuu (Sera Uratibu na Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, alisema wananchi wamejitolea lita 166 za damu, na kwamba watu 48 wamejitokeza kubaini ndugu zao na maiti 33 zimetambulika.

Alisema madaktari bingwa 10 kutoka hospitali za Mloganzila, Muhimbili jijini Dar es Salaam na Benjamin Mkapa jijini Dodoma wameshawasili katika Hospitali ya Rufani mkoani Morogoro kuendelea kutoa matibabu.

Aliongeza kuwa misaada mbalimbali imeendelea kutolewa ikiwamo mablanketi, dawa, vifaa tiba na elimu ya saikolojia kwa waathirika wa tukio hilo.

Baadhi ya wadau waliotoa misaada kwa majeruhi hao ni Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, Islamic Foundation na wabunge wa majimbo ya jirani ambapo Abood aliyetoa vifaa mbalimbali vya kusaidia majeruhi.

Nao baadhi ya ndugu waliojitokeza kuwatambua ndugu zao, Emmanuel Bernald na Benadikto Emanus walisema hali ya miili hiyo ni mbaya na ni ngumu kuitambua na kuipongeza serikali kwa kuleta kifaa na wataalamu wa kuwatambua vinasaba ili waweze kubaini ndugu zao.

Kadhalika wameziomba mamlaka husika kutoa elimu ya magari ya mafuta pindi yanapoanguka mara kwa mara kwa jamii ili waweze kuepukana na majanga kama hayo kutokana na tukio kama hilo kujitokeza kwa mara ya tatu nchini.

## Vilio vyatawala maziko

INATOKA UK. 3

mara kwa mara kwa kuwa wapo waliokufa ambao walikwenda kuangalia.

Alisema wazazi wamepata hasara kwa kuwa waliokufa wengi ni vijana na kwamba mtoto wake alikuwa mchezaji wa mpira.

Miili hiyo ilianza kuzikwa majira ya saa 11 jioni, viongozi wa dini mbalimbali waliweka udongo kwenye makaburi namba 15 na kufuatiliwa kwa Waziri Mkuu aliongoza kuweka udongo kwenye majeneza matatu.

Baada ya hapo askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) walianza kuweka udongo kwenye makaburi hayo.

Wakati majeneza yenye miili ya waliofariki ikipangwa uwanjani, Waziri Mkuu akiwa ameongozana na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alielekea katika wodi walipolazwa majeruhi 15 wa ajali hiyo, na kupata maelezo kutoka kwa madaktari na majeruhi.

"Madaktari wanajitahidi, tuwe na imani tumwombe Mungu aendelee kuwalinda, tunaamini watapona, nimewajulia hali zao ni nzuri wakilinganisha na jana, tunaamini watarejea katika hali ya kawaida," alisema.

Majeruhi wengine walikuwa wamelazwa katika wodi ya macho ambayo iligeuzwa ya majeruhi baada ya ajali hiyo. Waziri Mkuu alitembelea kitanda kimoja baada ya kingine na kuzungumza na majeruhi ambao walisema wanaendelea vizuri na kueleza wanaridhishwa na huduma zinatolewa hospitalini humo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**GARI INAUZWA,** Toyota Land Cruiser Amazon Vx DIESEL AUTOMATIC no 'C' safi sana Bei 27 milion. Leyland DAf Tank ya maji Diesel Lita elfu 10 inatembea safi sana Reg. namba D bei ni Sh. 28 milion. Mawasiliano: 0713 227788/ 0713 469480

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

### PASIPOTI IMEPOTEA



**Edwin Ohuru Abuya** anatangaza kupotelewa na hati yake ya kusafiria (passport) yenye **Na. AB 227417** iliyotolewa na idara ya Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2007 .

**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.**

**Taarifa ya polisi: MPA/RB/8883/2016**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**MAHAKAMA YA MWANZO BUSANGI,**
**WILAYA YAKAHAMA.**

**YAH:- KUITWA SHAURINI.**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Busangi,wilaya ya Kahama.**

**Shauri la Talaka namba 04/2019.**
**MDAI......ALEN KIJA STEPHANO**
**dhidi ya MDAIWA.... GRACE MABONDO.**
**Kwa GRACE MABONDO – popote ulipo.**

Alen Kija Stephano amefungua shauri la madai ya Talaka dhidi yako Grace Mabondo katika **MAHAKAMA YA MWANZO BUSANGI,**iliyopo wilayani Kahama.

Shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 26/08/2019 saa 3:00 Asubuhi.Unatakiwa kufika Mahakamani bila kukosa.

AMRI hii imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa MAHAKAMA YA MWANZO BUSANGI leo tarehe 05/08/2019.

**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo hii tarehe 05/08/2019.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,


au piga simu: 0767 223311

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# GUARDIOLA:
## VAR IMEBADILISHA NGUVU YA MCHEZO

**LONDON, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kwamba matumizi ya teknolojia ya kusaidia maamuzi kwa njia ya video, VAR, hubadilisha "nguvu" ya michezo baada ya kikosi chake kuibuka na ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya West Ham juzi Jumamosi, ambapo mshambuliaji Gabriel Jesus alikuwa mchezaji wa kwanza wa Ligi Kuu bao lake kukataliwa.

Wakati wakiwa wanaongoza kwa mabao 2-0, Jesus alifunga bao lililodhaniwa kuwa ni la tatu kwa City, lakini mwamuzi, Mike Dean alilikataa bao hilo kuwa ni la kuotea baada ya kuitumia VAR.

Huu ni msimu wa kwanza teknolojia hiyo kutumika kwenye Ligi Kuu ya England na VAR ikatumika tena kwenye mchezo huo, wakati penalti ya Sergio Aguero ilipookolewa na kulazimika kuipiga tena.

"Unatakiwa kuwa imara kiakili wakati VAR inapokuwa haipo upande wako," alisema Guardiola akiiambia BT Sport.

"Unafikiri kwenye mchezo unaongoza kwa 3-0, lakini kumbe matokeo yanasema 2-0, kwa hakika mchezo unakuwa tofauti kabisa.

"Unatakiwa kuwa mtulivu na imara. Inakwenda kubadilisha nguvu sio tu kwa timu, lakini pia kwa watangazaji. Litakuwa somo zuri kwa siku zetu za usoni."

VAR ilikuwa sababu kubwa ya City kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita, maamuzi ambayo yalikataa bao la dakika za mwisho la Sterling ambalo lingewapeleka robo fainali dhidi ya Tottenham.

"Baada ya kile kilichotokea kwenye mchezo dhidi ya Tottenham kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa sasa angalau tunaweza kutuliza hisia zile," amesema Guardiola.

## GRIEZMANN AIFUNGIA KWA MARA YA KWANZA BARCA

**MICHIGAN, Marekani**


BARCELONA ilitumia dakika 15 za kipindi cha pili kushinda mabao 4-0 kwenye dimba la Michigan juzi Jumamosi mbele ya mashabiki zaidi ya 60,000.

Luis Suarez alifunga mara mbili kwenye mchezo huo na kufikisha mabao matatu aliyofunga kwenye maandalizi ya msimu mpya, huku pia Barca walishuhudia bao la kwanza la Antoine Griezmann tangu aliposajiliwa kwa euro milioni 120 kutoka Atletico Madrid mapema kipindi cha majira ya joto. Ousmane Dembele alikamilisha idadi ya mabao kwa kufunga la nne.

Ushindi huo wa Barca umekuja siku tatu baada ya kuwafunga Napoli 2-1 mjini Miami na kuifanya ziara yao ya nchini Marekani kuwa bora zaidi kwao.

Huku Lionel Messi akiwa ameumia pale Ann Arbor, Ernesto Valverde alitaja kikosi imara kwa ajili ya mchezo wa ufunguzi dhidi ya Athletic Bilbao katika dimba la Mames siku sita zilizopita.

Miamba hao wa Hispania haraka walitawala mchezo huo, huku Frenkie de Jong akimiliki kiungo ya kati, huku Nelson Semedo na Dembele wakitawala winga ya kulia na Griezmann akifanya yake kule winga ya kushoto.



## DE GEA BADO HAKIJAELEWEKA MAN UNITED

**MANCHESTER, England**



GAZETI la The Mirror limebainisha kwamba majaliwa ya golikipa wa Manchester United, David de Gea bado yapo shakani.

Gazeti hilo limedai kwamba, raia huyo wa Hispania bado hajakubali kusaini mkataba mpya wa kuendelea kukaa hapo kwenye dimba la Old Trafford.

Mapema mwezi uliopita ilidaiwa kwamba kipa huyo mwenye umri wa miaka 28 amekubali kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ambao unamfanya alipwe kiasi cha pauni 350,000 kwa wiki.

Lakini taarifa za sasa zinasema kwamba, mazungumzo hayo hayakuweza kufikia makubaliano kati ya wawakilisha wa De Gea na maofisa wa Man United.

Hivyo basi ESPN FC imeripoti kuwa klabu kubwa Ulaya kama Paris Saint-Germain na Real Madrid zitaingia tena sokoni kwa ajili ya kuwania saini ya kipa huyo.

Kipa huyo wa zamani wa klabu ya Atletico Madrid, De Gea atakuwa huru kuzungumza na klabu yoyote mwishoni mwa mwaka huu na anaweza kusaini makubaliano ya awali na kumfanya kumuacha kocha Ole Gunnar Solskjaer kulazimika kuingia tena sokoni kipindi kijacho cha majira ya joto.

## HABARI MICHEZO



Baadhi ya Yosso wa Kiafrika waliodhaminiwa na Kampuni ya QNET wakipata mafunzo pamoja na wenzao katika Klabu ya Manchester City. **PICHA: QNET**

# QNET YADHAMINI YOSSO WA AFRIKA SHULE YA SOKA MAN CITY

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inakuza soka la Afrika, kampuni ya mauzo ya moja kwa moja ya QNET ambayo ni mshirika rasmi wa klabu ya soka ya Manchester City, ikiwa kama sehemu ya ahadi yake ya kuendeleza vipaji na kurudisha kwa jamii, imedhamini wachezaji watatu chipukizi wa kiafrika kuhudhuria mafunzo ya mpira wa miguu ya jijini Manchester (City Football Language School in Manchester).

Shule ya Lugha ya Soka ya Manchester ni kozi ya wiki mbili ya mpira wa miguu na mafunzo ya lugha ya Kiingereza kwa wachezaji chipukizi (vijana). Kozi hiyo ilianza Julai 28 na inakamilika leo Agosti 12.

Akizungumza kuhusu fursa hiyo, Biram Fall, Meneja Mkuu wa QNET wa Kanda ya Kusini mwa Jangwa la Sahara alisema, wachezaji hao chipukizi walichaguliwa kutoka katika mchakato wenye ushindani mkubwa nchini Ghana, Cameroon na Ivory Coast, na kunufaika na kozi hiyo ambayo haina gharama yoyote kwao.

Alisema Shule ya Lugha ya Soka ni kozi ya lugha ya Kiingereza na soka yenye hamasha kwa wachezaji chipukizi wa umri wa kati ya miaka 12-17, ambayo inafanyika katika viwanja vya mafunzo vilivyoko Jiji la Manchester.

Aidha, alifafanua kuwa wachezaji chipukizi waliochaguliwa wanapata fursa ya kupata falsafa ya mafunzo na mbinu za soka za Manchester City kupitia katika vipindi vya mafunzo ambavyo vinaongozwa na makocha wa mpira wa miguu wa Jiji la Manchester.

Kadhalika, alisema wanapata fursa ya kuendeleza uwezo na ujuzi wao wa kutumia lugha ya Kiingereza kupitia majadiliano katika vipindi vya ulimwengu wa soka (the world of football) kutoka kwa walimu wa vituo vya mafunzo ya lugha vya British Study Centres.

Wachezaji hao chipukizi wanajifunza na kupata mafunzo nyumbani au katika makao makuu ya Manchester City katika Uwanja wa Etihad, sehemu ambayo watakuwa na nafasi ya kutumia miundombinu bora. Mafunzo hayo ya soka yenye ubunifu wa kiwango cha juu na mtaala wa Lugha ya Kiingereza yameandaliwa kwa lengo la kuhakikisha wanaongeza uwezo wa kujifunza nje na ndani ya uwanja, huku yakigusa maeneo ya msingi ya maisha ya mtaalamu wa mpira wa miguu.

Zaidi ya kutambuliwa na Shule ya Lugha ya Kiingereza ya British Council, kozi hii vile vile inatambuliwa na Eaquals ambao lengo lao ni kuthibitisha kwamba viwango vya juu katika kufundisha lugha na mafunzo vinafikiwa duniani kote.

"QNET inaendelea kuwekeza katika kuendeleza na kukuza vipaji katika ngazi zote. Udhamini wa Klabu ya Manchester City kama mshirika wa mauzo ya moja kwa moja ni moja kati ya majukumu yetu katika mpira wa miguu na ari ambayo mpira huo unaambatana nao duniani kote. Mchezo wa mpira wa miguu unaunganisha watu kutoka katika asili na maeneo mbalimbali.

"Mpira wa miguu vile vile unahamasisha kufanya kazi kwa pamoja kama timu, kuwa na ari ya timu, kufanya kazi kwa nguvu na hamasa. Hizi ni baadhi ya tunu za msingi za QNET kama biashara."

Kwa Afrika, QNET ni mshirika wa mauzo ya moja kwa moja Ligi ya Mabingwa, Kombe la Shirikisho la Total CAF na Kombe la Total CAF Supa Cup.

Novemba 2018, Kampuni ya QNET ilitunukiwa tuzo ya e-Commerce CSR Company kuwa ni kampuni bora ya biashara ya mtandao kwa mwaka huo, ambayo ilitolewa na Kituo cha Uwajibikaji wa Mashirika kwa Jamii cha Afrika Magharibi (Centre for Corporate Social Responsibility West Africa).

## Martial kubeba mikoba ya Lukaku Man United

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema Anthony Martial atakuwa mshambuliaji wake kiongozi msimu huu baada ya kumkabidhi jezi namba 9 baada ya kuuzwa kwa Romelu Lukaku.

Kocha huyo amesema kwamba anaamini kwa kiasi kikubwa kwamba Martial atamaliza tatizo la kufunga kwenye kikosi hicho na kuwafanya kutokuwa na ukame wa mabao kama inavyodhaniwa kwa sasa baada ya Lukaku kutimkia Inter Milan.

Kocha huyo anaamini Martial ni mtu sahihi wa kucheza katikati na hapo kwenye fowadi ataunda pacha na Marcus Rashford.

Katika kipindi ambacho Lukaku alikuwa kwenye kikosi hicho, Martial alikuwa akicheza upande wa kushoto.

Mashabiki wa Man United wanafurahia kwa timu hiyo kumpiga chini Lukaku, ambaye katika kipindi cha misimu miwili amefunga mabao 42 akicheza mshambuliaji wa kati.

Ndani ya kipindi hicho, Rashford amefunga mabao 26 na Martial mabao 23, lakini tofauti ni kwamba wawili hao walikuwa wakishambulia kutokea pembeni.

Solskjaer alisema: "Sawa, Rom amekuwa na rekodi nzuri hasa anapocheza mshambuliaji wa kati. Lakini, nina hakika tutafunga mabao ya kutosha tu kutoka kwa Anthony Martial, Marcus Rashford, Dan James na Jesse Lingard."

## Lewandowski ataka Bayern isajili zaidi

**MUNICH, Ujerumani**

BAADA ya Bayern Munich kupata kipigo kutoka kwa wapinzani wao wa soka la Ujerumani, Borussia Dortmund kwenye mchezo wa kombe la Super, mshambuliaji Robert Lewandowski anataka kikosi chao kiimarishwe kwa kusajili wachezaji zaidi.

Beyern ilifungwa na Borussia kwenye mchezo huo wa kombe la Super ambao ni ishara ya ufunguzi wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.


Lewandowski ambaye ni nahodha wa timu ya taifa ya Poland ameliambia gazeti la Bild kuwa anataka klabu yake kusajili wchezaji bora ambao wataweza kuleta athari ya haraka kikosini hapo.

Nyota huyo amelalamikia ukosefu wa wachezaji wanaoweza kubadili mchezo miongoni mwa wachezaji wa akiba wa Bayern na amehoji sera ya uhamisho ya klabu hiyo.

"Bila shaka wachezaji chipukizi katika benchi wana uwezo, hii ni kweli, lakini wakati mwingine unahitaji mchezaji mwenye uwezo mkubwa wa moja kwa moja ambaye anaweza kuingia uwanjani na kuisaidia timu," alisema Lewandowski.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CEBALLOS ANA UBORA WA ARSENAL- EMERY

●●●Mtazamo wake ni mzuri na ametuonyesha malengo yake na njaa kubwa ya mafanikio...

**LONDON, England**

UNAI Emery amezungumzia mawazo ya usajili wa Dani Ceballos kipindi cha majira ya joto kwa mkopo kutoka Real Madrid huku jana alitumaini kumwanzisha kuichezea Arsenal kwa mara ya kwanza dhidi ya Newcastle.

Arsenal jana ilisafiri kwa ajili ya mchezo wao huo wa ufunguzi wa Ligi Kuu msimu huu, huku nyota wao waliowasajili kipindi hiki cha majira ya joto wakipigania kuwa fiti.

Ceballos, ambaye alisajiliwa kwa mkopo wa muda mrefu kutoka Madrid, jana alitarajiwa kuanza kucheza mechi yake ya kwanza ya mashindano, lakini ilitegemewa kama kiungo huyo alikuwa amepona vizuri baada ya kuumia kifundo cha mguu wakati wa mchezo wa kipigo wa maandalizi ya msimu mpya dhidi ya Barcelona wikendi iliyopita.

"Akili ya Ceballos iko imara," alisema Emery akimzungumzia mchezaji huyo aliyeicheza mechi sita timu ya Taifa ya Hispania.

"Mtazamo wake ni mzuri. Jumapili wakati alipoumia kifundo cha mguu nilifikiri 'amevunjika mguu'.

"Lakini baadaye Jumatatu alifanya mazoezi - (alisema) 'Nipo vizuri na nataka kufanya mazoezi'. Anatuonyesha malengo yake na njaa yake kubwa ya mafanikio. Nafikiri tunahitaji wachezaji kama hawa."

Aidha, Unai alisema kabla ya mchezo wa jana alikuwa anafuatilia na kuangalia kwa ukaribu ufiti wa washambuliaji wake, Nicholas Pepe na Alexandre Lacazette kabla ya kuivaa Newcastle, na alibainisha kuwa Pepe angeweza kuanza kuichezea klabu hiyo.

Emery aliiongoza Arsenal kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi msimu uliopita, akiikosa nafasi ya nne kwa pointi moja na pia walifungwa kwenye fainali ya Kombe la Europa na wapinzani wao wa jiji moja la London, Chelsea.

Lakini kwa sasa klabu hiyo pamoja na Ceballos, imewasajili David Luiz, Pepe, Kieran Tierney, Gabriel Martinelli na William Saliba (ambaye amepelekwa kwa mkopo Etienne kule Ufaransa).

Arsenal imewanunua wachezaji watano kipindi hiki cha majira ya joto na Kocha Emery amesema ana hamasa kubwa kufanya kazi na wachezaji wake wapya aliowasajili pamoja na vijana alionao.

Huku Saliba akibakia akicheza kwa mkopo wa muda mrefu kule St Etienne, waliobaki watakuwa na kazi kubwa ya kumsaidia Emery kuwa na matokeo mazuri zaidi msimu huu na anaamini timu yake imekuwa bora zaidi kuliko ile aliyoirithi mwaka mmoja uliopita.

"Tunafuraha kubwa na tuna hamasa nzuri kwa kile klabu ilichokifanya kwenye dirisha la usajili," alisema.

"Pia (Mkuu wa soka) Raul Sanllehi na (Mkurugenzi wa soka) Edu walikuwa wanafanya kazi pamoja kupata suluhisho bora, kuwa timu yenye ushindani na kuweza kumsajili mchezaji mwingine na pia kuitumia klabu kwenye kuimarisha uchumi wetu."

## KWA UFUPI

**JUVE YAENDELEZA KWA POGBA**

Juventus haijanyosha mikono juu kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, 26. ***(Express)***

**MODRIC, NEYMAR KUPISHANA**

Paris St-Germain inavutiwa na mpango utakaoshuhudia Real Madrid ikimnunua mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27, kwa kubadilishana na kiungo Mcroatia Luka Modric, 33, pamoja na dau la pauni milioni 149. ***(Times)***

**PSG YAMKATAA BALE**

Real Madrid imetoa ofa ya pauni milioni 85 na mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 30, ili kumpata Neymar majira haya ya joto lakini dili hilo limekataliwa na PSG. ***(Mundo Deportivo, via Express)***

**PERISIC AKARIBIA BAYERN**

Bayern Munich inakaribia kumsajili kiungo Mcroatia Ivan Perisic, 30, kutoka Inter Milan. Klabu hizo mbili zinakamilisha makubaliano ambayo yatashuhudiwa mchezaji huyo akihama awali kwa mkopo kwa makubaliano ya kumnunua kwa pauni milioni 23.5. ***(Sky Italia via Sky Sports)***

**AURIER ATAKA KUTIMKA SPURS**

BEKI wa Tottenham, Serge Aurier anataka kuondoka klabuni hapo, na AC Milan na PSG zote zinavutiwa kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast. ***(Mail)***

**DE GEA AITESA UNITED**

Manchester United bado hajajua endapo kipa David de Gea atatia saini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia. Mkataba wa kipa huyo wa kimataifa unamalizika majira ya joto yajayo na atakuwa huru kuzungumza na klabu nyingine nje ya England kuanzia Januari. ***(Mirror)***

**BECKHAM KUMPA ULAJI MOYES**

KOCHA wa zamani wa Everton na Manchester United, David Moyes yopo katika orodha ya wanaotakiwa kuinoa klabu ya David Beckham, Inter Miami. ***(Mirror)***

**MOURINHO AIBUKIA SKY SPORTS**

Jose Mourinho amegeukia jukumu la uchambuzi katika Kituo cha TV cha Sky Sports na kazi yake ya kwanza ilikuwa jana Jumapili kati ya timu yake ya zamani Manchester United dhidi ya Chelsea. ***(Sky Sports)***

**DYBALA HAKIJAELEWEKA PSG**

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Argentina, Paulo Dybala, 25, amesafiri na timu yake kwa ajili ya mechi ya mwisho ya maandalizi ya msimu mpya dhidi ya Atletico Madrid itakayopigwa Stockholm, Sweden licha ya kuwindwa na miamba ya Ufarasa, Paris St-Germain. ***(Mail)***

**KHEDIRA AITIBUA JUVENTUS**

Juventus imekerwa na kitendo cha kiungo Sami Khedira, 32, kufuatia Mjerumani huyo kukataa ofa kadhaa ikiwa ni pamoja na kujiunga na Wolves - akitaka kusubiri ofa kutoka Arsenal ambayo ilishindwa kukamilika. ***(Calciomercato via Sun)***

**BOLASIE AZIVUTIA CELTIC, BESIKTAS**

Celtic, Besiktas na Rennes zote zinafukuzia huduma ya winga wa Everton na DR Congo, Yannick Bolasie, 30, ambaye tayari ameshakataa wazo la kutua CSKA Moscow ya Urusi. ***(Goal)***



# TANZANITE MABINGWA WAPYA COSAFA U-20

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), imefanikiwa kuutwaa ubingwa wa mashindano ya Cosafa baada ya kuwafunga wenzao wa Zambia mabao 2-1 katika mchezo wa fainali uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Wolfson mjini Port Elizabeth.

Mabingwa hao wapya walienda mapumziko wakiwa mbele kwa bao 1-0 katika mchezo huo uliochezwa jana mchana nchini Afrika Kusini.

Tanzanite ambayo ni timu mwalikwa katika mashindano hayo, imetwaa ubingwa huo kwa mara ya kwanza ikiwa na Kocha Mkuu Mtanzania Bakari Shime ambaye anasaidiana na kiungo wa zamani wa timu ya Taifa ya Wanawake maarufu, Twiga Stars, Edna Lema.

Bao la kwanza la Tanzanite lilifungwa na mshambuliaji wa Simba Queens, Opa Clement dakika ya 24 katika mchezo huo ambao timu zote zilicheza kwa kukamiana.

Zikiwa zimebakia dakika tatu ili mchezo huo umalizike, mshambuliaji, Protasia Mbunda alifunga bao la ushindi na kuinyamazisha Zambia ambayo iliwafungwa Tanzanite katika hatua ya makundi kwa mabao 2-1.

Tanzanite iliyokuwa katika Kundi B ilitinga hatua ya fainali baada ya kuwachapa wenyeji Afrika Kusini mabao 2-0 wakati Zambia yenyewe iliwafunga Botswana goli 1-0.

Shime alisema kujituma na kutokata tamaa kwa wachezaji wake ndio kumeifanya timu hiyo ipate ushindi katika michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Kocha huyo aliongeza kuwa, ushindani ulioongezeka kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania na Ligi Daraja la Kwanza, ndio imechangia kupata wachezaji wenye uwezo mzuri na wenye kiu ya mafanikio.

Kikosi cha Tanzanite kinatarajia kurejea nchini leo huku dada zao Twiga Stars wakijiandaa kuelekea Nairobi kucheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya wenyeji Kenya utakaochezwa Alhamisi Agosti 15 mwaka huu.




Mwandaaji wa mashindano ya soka ya Suguye Cup, Nabii Nicolaus Suguye, akimvalisha medali mmoja wa wachezaji wa timu ya Fairplay baada ya kuutwaa ubingwa wa michunao hiyo juzi Jumamosi kwa kuifunga timu ya Kivule Fores mabao 2-1. **MPIGAPICHA WETU.**

# Kaseja afunguka AS Kigali itafia Dar

**Na Shufaa Lyimo**

KUFUATIA sare tasa katika mchezo wao wa kwanza wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Kigali, Nahodha wa Klabu ya KMC FC, Juma Kaseja amesema wana nafasi nzuri ya kurekebisha makosa yao na kushinda mechi ya marudiano wiki mbili zijazo hapa nchini.

Akizungumza na Nipashe juzi kutoka Kigali, Kaseja alisema kwa ujumla timu yao ilijitahidi kutokana na ushindani mkali katika mechi hiyo.

**"Japokuwa tumepata sare ugenini bado tuna dakika 90 ambazo tutazitumia vizuri kwenye mchezo wetu wa marudiano,"alisema Kaseja.**

Hata hivyo, aliongeza kuwa kikosi chao kilichocheza kilikosa baadhi ya nyota wao kutokana na vibali vyao vya kimataifa (ITC) kuchelewa, lakini akasifu juhudi zilizoonyeshwa na wachezaji waliocheza.

Kaseja pia aliwashukuru Watanzania kwa ujumla kwa ushirikiano mkubwa walioonyesha wakati wakiwa Rwanda na kuwaahidi kufanya makubwa kwenye mechi ijayo hapa nchini.

Endapo KMC itafanikiwa kusonga mbele, itakutana na mshindi kati ya Proline FC ya Uganda anapotokea kocha wao, Jackson Mayanja na Masters Security Services ya Malawi.

# Michuano ya Suguye Cup yamkuna Nabii

**Na Mwandishi Wetu**

MWANDAAJI wa mashindano ya soka ya Kombe la Suguye, Nabii Nicolaus Suguye, amesema lengo la michunao hiyo ni kuwahamasisha, kuibua vipaji na kuwaweka pamoja vijana ili kutojihusisha na maovu mitaani limetimia.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawazi kwa washindi wa mashindano hayo, Suguye alisema alianzisha michuano hiyo maalumu kwa ajili ya kuwasaidia vijana kuepukana na kujiingiza kwenye matukio ya uovu na pia kuibua vipaji vya soka kwa vijana.

"Naweza kusema kwamba malengo yangu ya kuanzisha mashinano haya yamefikiwa, kwani tumeshuhudia timu zenye vijana wenye vipaji vya ukweli wakishindana kwa pamoja kuhakikisha wanaibuka na ushindi," alisema Nabii Suguye.

Aliongeza kusema kuwa mashindano hayo pia yamesaidia kuibua vipaji vya wachezaji wapya vijana ambao ana uhakika watawezа kujiimarisha zaidi na wengine kuchukuliwa na timu kubwa za Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza nchini.

"Kama mnavyojua kwamba mchezo wa soka kwa sasa ni moja ya ajira kubwa zaidi duniani, hivyo naamini wachezaji walioibuliwa kupitia michuano hii wataweza kusajiliwa na timu kubwa," alisema.

Katika mashindano hayo timu ya Fairplay ya Kivule jijini Dar es Salaam ambayo msimu huu itashiriki Ligi Daraja la Nne, iliibuka mabingwa baada ya kuifunga Kivule Fores mabao 2-1 kwenye fainali iliyopigwa viwanja vya Shule ya Msingi Misitu Kivule.

Mashindano hayo yalianza kutimua vumbi mwanzoni mwa Julai na kufikia tamati juzi Jumamosi na timu ya Fairplay kuibuka wafalme wa kwanza wa mashindano hayo yaliyoshirikisha timu 24 kutoka maeneo yanayounganisha Jimbo la Ukonga la Kanisa la WRM chini ya kiongozi wake, Nabii Suguye.

# Namungo yapania vigogo Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikitarajiwa kuanza Agosti 23, mwaka huu, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hitimana Thiery, amesema hana hofu na ushindani uliopo hususan kutoka kwa vigogo wa ligi hiyo.

Namungo FC itashiriki Ligi Kuu Bara kwa mara ya kwanza, lakini kocha Thiery amesema maandalizi waliyoyafanya yanampa matumaini ya kufanya makubwa ligi ikianza.

"Kikosi chetu kina ari ya kutosha kabla ya ligi kuanza, hivyo ni imani yetu tutafanya makubwa msimu utakapoanza hasa ukizingatia tumepambana kupanda daraja. "Hakuna timu tunayoihofia kwenye ligi hata hao vigogo ambao ni Simba, Yanga, Azam na timu nyingine zaidi ya kuziheshimu kwa kuwa tumezikuta ila tutakapokutana nao uwanjani lazima tuonyeshe kuwa tupo tofauti," amesema Thiery.

# Michezo



Jumatatu Agosti 12, 2019

**Nipashe**

## Ceballos ana ubora wa Arsenal- Emery

HABARI UK 30

**KITU HICHO...**




Mshambuliaji wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang akiifungia timu yake bao pekee wakati ikishinda 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle United iliyopigwa Uwanja wa St. James' Park jana. **PICHA: MTANDAO**

# ZAHERA: SABABU YANGA KUSHIKWA TAIFA NI HIZI

●●●Asema 2-1 ugenini inawezekana, aipeleka kuzoea baridi Kilimanjaro na kujipima kwa FC Leopards ya Kenya...

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kujikuta timu yake ikilazimishwa sare nyumbani kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera amekichambua kikosi chake na kuanika eneo la kuboresha ili kuweza kupata ushindi mechi ya marudiano ugenini.

Yanga ilishindwa kuibuka na ushindi nyumbani katika Uwanja wa Taifa juzi baada ya kutoka sare ya bao 1-1, ambapo ililazimika kusubiri hadi dakika ya 86 kusawazisha bao la dakika ya saba la wageni wao, kwa mkwaju wa penalti kupitia kwa Patrick Sibomana.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera, akizungumza baada ya mechi hiyo alisema bado kikosi chake hakijawa na maelewano mazuri jambo ambalo liliwapa tabu kupata matokeo katika mechi hiyo.

Zahera alisema tatizo kubwa lilikuwa katika safu ya ushambuliaji na kwamba ilishindwa kuwa makini kwa kutumia nafasi walizopata, licha ya kwamba wapinzani wao pia walikuwa wazuri na wenye kasi.

"Bado ninaamini tunaweza kupata matokeo ugenini kwa kushinda mabao hata 2-1, kwa wiki mbili zilizobaki kabla ya kurudiana, tunaweza kuzitumia kufanya marekebisho hususan safu ya ushambuliaji.

"Lengo ni kuwa na kikosi imara ambacho kitapata matokeo kwenye mchezo wetu wa marudio, mashabiki waendelee kutupa sapoti, nami nitafanyia kazi makosa yote," alisema.

Yanga ambayo kesho itaelekea mkoani Kilimanjaro kujiandaa na mechi hiyo, itarudiana na mabingwa hao wa Botswana kati ya Agosti 23-25 na mshindi wa jumla atakutana na mshindi wa jumla kati ya Green Mamba ya Eswatini (zamani Swaziland) na Zesco ya Zambia.

Katika kujiandaa na mechi hiyo, Yanga kesho inatarajiwa kuelekea mkoani Kilimanjaro kuweka Kambi kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano ikiwa ni pamoja na kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya FC Leopards ya Kenya.

Akizungumza na Nipashe jana, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya klabu hiyo, Saady Khimji alisema, wakiwa Kilimanjaro watacheza mechi ya kirafiki Agosti 16 dhidi ya Polisi Tanzania kabla ya siku mbili baadaye kupimana ubavu na FC Leopards mkoani Arusha.

"Maandalizi kwa ajili ya michezo pamoja na kambi yanaendelea vizuri, tumeamua kupeleka timu Kilimanjaro kwa sababu mchezo wetu ujao tutacheza ugenini na kuna hali ya baridi ili wachezaji wazoee hali ya hewa," alisema Saady.

Alisema lengo kubwa ni kuhakikisha Yanga inasonga mbele pamoja na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu ujao.

# Aussems atoa siri UD Songo kufia Dar

**Na Mwandishi Wetu**


KUFUATIA matokeo ya sare tasa ugenini Msumbiji dhidi ya UD Songo kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, ametoa sababu zinazoweza kuwapa ushindi watakaporudiana wiki mbili zijazo Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Simba baada ya mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Beira, Msumbiji juzi, ilirejea jijini Dar es Salaam Jumamosi usiku na jana kikosi hicho kilifanya mazoezi mepesi kuelekea kujiandaa na mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC utakaochezwa Agosti 17, mwaka huu Uwanja wa Taifa.

Akizungumzia mechi hiyo, Aussems alisema ana uhakika wanaweza kupata matokeo nyumbani dhidi ya UD Songo kutokana na kuwa mbele ya mashabiki wao na ubora wa Uwanja wa Taifa.

"Ulikuwa mchezo wa wazi, walikuwa wakijaribu kufunga na kwetu ilikuwa hivyo, jambo muhimu hatujaruhusu bao. Mchezo wa marudiano utakaochezwa Dar ni muhimu sana, kwa ushangiliaji wa mashabiki wetu na uwanja mzuri nafikiri tutafanya vizuri," alisema Aussems baada ya mchezo dhidi ya UD Songo.

Alisema kwa sasa wanajiandaa na mechi dhidi ya Azam FC, maandalizi ambayo yanakwenda sambamba na mchezo wa marudiano dhidi ya UD Songo utakaopigwa kati ya Agosti 23-25.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >